

JUU YA MBAWA ZA HUA MWEUPE KAMA THELUJI



Na tuinamishe vichwa vyetu:

Bwana mpendwa, twakushukuru usiku huu kwa ahadi ya kuja kwake Bwana Yesu, ambako tutakutanika katika mkutano mkuu ambao hautakwisha, kwa furaha na nyimbo, tutakapokusifu kote katika nya—nyakati zisizo na mwisho zijazo. Tunaomba baraka zako juu ya mkutano huu usiku wa leo. Tunaomba baraka zako juu ya maskani haya, juu ya watumishi wake, wachungaji wake, watendaji pamoja nayo, wachungaji wasaidizi, na wengine wote.

² Twakuomba uwabariki hawa, Bwana, ambao wamesafiri maili nyingi kuhudhuria mkutano huu, wawekelee mkono Wako wa rehema wanaposafiri kurudi manyumbani mwao. Tujalie, Bwana. Na tukutane mara nyingi zaidi pamoja katika mahali hapa panapoitwa nyumba ya Mungu, kuabudu. Wabariki wale ambao wanasikiza usiku huu, Bwana, kwa njia ya simu. Na kila mtu asiyeokolewa ampate Yesu Kristo Mwokozi wao, usiku huu; waponye wagonjwa wote na wanaoteseka. Baba, mtumishi wako anaingia kwa utumishi, katika Jina la Yesu. Amina!

³ Bwana abariki kila mmoja wenu. Nina furaha sana kuwa hapa usiku huu. Naliingia tu wakati Ndugu Ernie alikuwa akiimba sehemu ya mwisho ya wimbo wake, *Juu ya Mbawa za Hua*. Bila shaka ni shairi nzuri, ni nzuri, bila shaka, na na-najua limekuja wakati unaofaa. Kwa hivyo sasa, tunashukuru sana.

⁴ Na kwenu nyote mnaonisikiza usiku huu nchini mwote, laiti mngalikuwa hapa muone huku kungoja, matumaini juu ya nyuso za watu hawa waliojazana humu jengoni usiku huu; wakiwa na wakati wa ajabu.

⁵ Tunataka kumshukuru Ndugu Jack Moore, na Dada Moore, na Ndugu Noel, Ndugu Bootlayer, Ndugu Brown, hawa wote wanaoshirikiana nao maskani nzima, watumishi wote, kwa kutualika tena.

⁶ Ilikuwa...bila shaka...kama...singesema ni kwa ulinganifu, ilikuwa tu ni mkono wa Mungu uliotenda kazi. Kuna ndugu fulani hapa aliyekuwa na ndoto wakati mfupi uliopita, kuhusu kutendeka kwa jambo hili, kasema, mimi nilikuwa nimesimama huku nimevalia suruali ndefu, nimevalia viatu vya kihindi vya ngozi ya kulungu." Na hivyo ndivyo hasa nilikuwa nimesimama nilipomwita Ndugu Jack akahudhurie mkutano huu, vivyo hivyo hasa (kule Carson Colorado) viatu vya kihindi na suruali ndefu nyeupe ya aina ya Levi; Ndugu Leo, iwapo

unasikiza, nilikuwa nitakutana nawe katika dakika chache tu. Kwa hivyo hapo ndipo huu mkutano ulipopangwa, papo hapo.

⁷ Sasa ni Jumapili usiku; najua wengi wenu mtasafiri usiku mzima mkielekea makwenu, wengine wenu watasafiri asubuhi. Mimi nina safari ya siku mbili kwa motokaa mbele yangu. Na kwa hivyo hatu—hatutawakawisha kwa muda mrefu sana. Na nimejaribu kuufanya huu usiku wa kikale, usiku ambao Ndugu Brown, na Ndugu Jack, na sisi wote tulizoea kuwaombea wagojwa miaka kadha iliyopita, tutawaombea wangojwa jinsi tulivyokuwa tukiwaombea wakati huo.

⁸ Basi, mwaweza kunisikia huko nyuma? Nazidi kuzishusha hizi maikrofoni kwa maana sauti imenipwelea.

⁹ Na kwa hivyo nataka ku... Jambo fulani dogo tu, tukio hili dogo lilitukia. Naam, wao walikuwa wakiniambia muda mchache uliopita ya kwamba kulikuweco ndugu fulani, huenda yuko hapa mkutanoni usiku huu, ambaye ametoka hivi punde katika udhehebu; akaja kule Shreveport, alitaka kusikia Ujumbe. Naye akachanganyikiwa, hakujua alipokuwa, kwa hivyo akaenda mjini. Akaona watu wamekusanyika, akasema, “Je, hapa ndipo Billy Branham atahubiri?”

¹⁰ Akasema, “Sivyo, ni mahali Billy Graham anahubiri kwa—kwa njia ya sinema.”

¹¹ Akasema, “Vema, samahani, ni—niko mahali pasipofaa.”

¹² Akasema alikuja huku, akasema, “Sasa, niende wapi, Bwana?” Kasema alianza kuja kwa hii barabara kuu. Sijui inaitwaje, mna kanisa kubwa hapa mwisho wake. Barabara ya Texas. Na kulikuwa na msalaba mkubwa mweupe juu ya hilo kanisa. Kasema Bwana alimwambia, kasema, ‘Endelea kusonga mbele tu.’ Kasema... alipofika pale, kulikuweco na... Kasema, “Vema, lazima iwe hapa, mna motokaa nyingi sana zimesimama humu.” Naye kasema, “Bibi-arusi na Bwana arusi wakatoka humo kanisani.” Hiyo ilikuwa usiku wa leo, kulikuweco na arusi, niliwaona wakitoka. “Bwana akasema, ‘Sasa, hivyo ndivyo ilivyo. Unatoka katika udhehebu kuingia katika Bibi-Arusi, kuenda pamoja na Bwana-Arusi.’” Mwaona? Mnaona?

¹³ Nilikuwa nikinena na mke wangu, nilipokuwa nikija barabarani, jinsi mwezi na nyota zilivyokuwa zikining’inia juu ya huo msalaba, tulipokuwa tunaukaribia. Nakisia mimi hutazama mambo madogo kama hayo, labda kustahisha imani yangu katika Mungu pamoja na huduma yangu.

¹⁴ Nilikuwa nikiwaza usiku wa leo, kule Tucson, ilikuwa kwamba Victor La Deaux, yeye alikuwa huyu Mfaransa. yeye ni Mfaransa halisi. Naami ni nilikuwa nikiwaambia hivi majuzi, ya kwamba nilipomaliza kuhubiri, nikijaribu kutenganisha udhehebu na Ukristo halisi... Na mtu fulani alikuwa akinipa... habari fupi juu yake, kutoka kanisa mashuhuri la kidhehebu la Kipentekoste.

¹⁵ Na kwa hivyo Danny Henry, nafikiri yeye ni binamu wa mcheza sinema fulani au cho chote kile, naye alikuwa Mbatisti; yeye alikimbia jukwaani, na akanikumbatia kwa mikono na kusema, “Ndugu Branham, natumaini hii haitaonekana kama kukufuru, bali hayo yangaliweza kuwa sura ya 23 ya Ufunuo.” Na alipoanza kusema jambo jingine, akaanza kunena kwa lugha.

¹⁶ Na hili, Wafaransa watatu...Mwanamke Mfaransa (mwanamke mkubwa mweusi na mnene, kutoka Louisiana, huenda yuaketi hapa usiku huu) akayaandika kwenye kijikaratasi, yale huyo aliyoyasema. Kisha Victor La Deaux, muhudumu, akaandika jambo lile lile; nao walikuwa wakilinganisha maandishi hayo, au walikuwa wakitaka kufanya hivyo. Mtu mwenye nywele za rangi ya shaba akisimama kule nyuma kabisa, amekati nyuma sana alivyoweza, akaja humu, alitaka kuona maandishi hayo. Alikuwa mkalimani wa Kifaransa katika Umoja wa Mataifa. Na maandishi hayo yote matatu yalikuwa sawa.

¹⁷ Yalisema hivi:

Kwa sababu umechagua njia hii iliyo ngumu zaidi. . . Umeichagua, umechukua. . . umeichagua kwa hiari yako. (bila shaka twajua hayo, ilimbidi Musa kufanya chaguo lake)

(kasema) Hii ndiyo njia halisi na sahihi, kwa sababu ndiyo njia yangu.

Na ni—ni shauri tukufu vipi umekata! (kasema). . . Kwa sababu hii sehemu kubwa ya mbinguni inakungojea.

Na hili lenyewe ndilo litakalosababisha, na kutimiliza, ule ushindi mkuu katika Upendo wa Kiungu.

¹⁸ Yote matatu yalikuwa sawa. Nalifikiri nilikuwa nayo katika Biblia yangu usiku huu, (niliangalia mle ndani, sikuipata), ile nakala yake ya asili.

¹⁹ Danny Henry hajui. . . kama mimi, hajui Kiingereza kizuri, licha ya Kifaransa. Ukichunguza mle, ni kama lugha ya Kifaransa, wanaweka kiarifa mbele ya kisifa. Na tafsiri ya zote tatu ilifanana kabisa.

²⁰ Danny Henry hivi majuzi, alitengeneza. . . Huenda Danny anasikiza usiku wa leo. Victor la Deaux labda anasikiza, kwa sababu yuko Tucson. Nanyi watu huko Tucson kanisani, maskanini, maskani ya Tucson ambamo Ndugu Green ndiye mchungaji wake; Ndugu Victor La Deaux, nasikia yuko katika mkutano wa hema papo hapo chini ambapo Park Avenue inapougana na njia kuu ya 80, ikija huku. Na kama utakuwa huko kesho usiku na usiku unaofuata kwa muda wo wote utakaokuwa huko nenda ukamsikize; na huenda Danny yuko

pamoja naye. Na huenda ikawa wanasikiza kutoka Maskanini usiku huu, sijui.

²¹ Danny alienda Yerusalemu mara baada ya hayo, naye akasema alikuwa amelala mle kaburini ubaoni...ubao wa mwamba alimolala Yesu, mwili Wake kabla tu ya kufufuka kwake. Naye akasema, mara nikaingia mawazoni mwake; naye akasema alikimbia nje, akaanza kulia, na akatembea upande wa nje. Naye akaongozwa...Yeye ni mtu anayetengeneza vitu kwa mawe; mawe fulani, namaanisha. Kasema alienda mahali waliposema ndipo msalaba uliposhindiliwa chini, naye akaangusha...akavunja kipande kidogo cha jiwe kikubwa kama hivi...Oh, inchi moja mraba, ama cho chote kile; akakiweka mfukoni mwake, naye akijisikia akilete nyumbani.

²² Alipofanya hivyo, kitu fulani kikamwambia, “Mtengenezee Ndugu Branham jozi ya sijafu toka kwake.” Kwa hivyo akakiweka katika maji ya betri, nacho kikageuka rangi kutoka ya gange ya kawaida kikawa jiwe lekundu. Naye akatengeneza sijafu.

²³ Naye aliponipa hizo, hakuwa ameona hilo, bali kupitia kwa sijafu hizo mbili mna mstari ulionyoka na mwembamba. Nimezivalia usiku huu, kuwaombea wagonjwa. Mnaona, ra-rangi ya jiwe lekundu, kama damu inayotiririka; zenye mstari ulionyoka na mwembamba kutoka upande huu hata mwingine. Jinsi hasa unabii wake ulivyosema, “njia iliyonyoka na nyembamba”; Mwaona, katika huo unabii. Na nilimwonyesha hiyo.

²⁴ Danny, iwapo unasikiza, wewe ama Ndugu La Deaux, mmoja wenu, usiku huu utakuwa ule usiku wa mtindo wa kale ambapo tutawaombea wagonjwa. Nina furaha kutembea katika njia hii iliyonyoka na nyembamba, njia ya Injili, njia ya Neno, pamoja na Bwana wetu Yesu Kristo.

²⁵ Mungu awabariki nyote. Naam, ninyi ni wazuri sana kuzungumzia, nitazungumza kwa muda mrefu nami nitawakawisha hapa kwa muda mrefu sana. Billy alisema kulikuweco na watu kati ya mia tatu na mia nne watakaombewa, kwa hivyo itanibidi tu kuharakisha ujumbe wetu upesi iwezekanavyo, ndiposa niwaombee wagonjwa.

²⁶ Sasa, kwa watu walio huko Arizona, usiku wa Jumamosi ijayo, tuko kule (siwezi kamwe kukumbuka jina la huo mji) Yuma, Arizona, kwenye karamu. Kwa hivyo, kule California, tutakuja Jumapili asubuhi, huko Los Angeles na mahali ambapo imesemwa tungekuweco.

²⁷ Usiku huu, nataka kuchukua fungu moja toka katika Maandiko.

²⁸ Mwajuaje, nilikuwa nimeketi mkahawani leo, mkahawa wa Morrison; Ndugu Jack mkewe, mimi na mke wangu. Tulienda

kwenye Mkahawa wa Morrison kuwa na wakati mzuri pamoja, hatukuwa tumeenda kutembea, hao wanaweke hawakuwa wamekuwa pamoja kamwe. Kijana mmoja akanijia, jina lake ni Green, ni babaye Ndugu Pearry Green. Akasema, “Wajua, Ndugu Branham, ulikuwa ukinena kuhusu pini ya Johnny! usiku uliopita.” Hiyo bila shaka. . . Ni nini? Ni kibano kidogo cha chuma. Akasema, “Ulikuwa ukinena kuhusu ‘pini ya Johnny,’ kasema, “Nimekuletea ‘pini ya Johnny,’” Akanipa mimi.

²⁹ Naam, hiyo ndiyo “pini ya Johnny,” mabibi, hiyo haifai kwa nywele. Pini ya Johnny, yeye alisema—alisema ameitumia kwa miaka kadha, kushikilia kurasa za Biblia yake. Kwa hivyo akasema, “Nitakupa pini ya Johnny” halisi. Kwa hivyo, Ndugu Green, iwapo umo humu mahali fulani ama unasikiza, hiyo ndiyo “pini ya Johnny,” iliyo nzuri sana, huzishikilia vizuri.

³⁰ Sasa tunataka kuyaenda Maandiko sasa hivi. Nami nawatakeni mfungue pamoja nami sasa katika Zaburi 55, kisha pia Mathayo 3. Na somo langu usiku huu lilikuwa wimbo wa Ndugu Ernie: *Juu ya Mbawa za Hua Mweupe Kama Theluji*. Naam, sitaweza kufikia muhtasari wote wa maneno na Maandiko niliyo nayo hapa, kwa maana nitaruka baadhi yake, na kwa sababu niliahidi ujumbe huu.

³¹ Bwana akipenda, huko Yuma Jumamosi ijayo usiku, nataka kuhubiri juu ya: *Masharti ya kunyakuliwa* Bwana akipenda.

³² Katika Zaburi 53. . . samahani, Zaburi 55:

Ee Mungu, uisikilize . . . (ati nini? 55 naama, bwana)

Ee Mungu, uisikilize sala yangu . . . usijifiche nikuombapo rehema.

Unisikilize na kunijibu, nimetanga-tanga nikilalama na kuugua.

Kwa sababu ya sauti ya adui, kwa sababu ya dhuluma yake yule mvovu. Kwa maana wananitupia uovu, na kwa ghadhabu wananiudhi.

Moyo wangu unaumia ndani yangu, na hofu za mauti zimeniangukia. Kutohofu na tetemeko limenijia, na hofu kubwa imenifunikiza. Nikasema, Ningekuwa na mabawa kama njiwa, ningeruka mbali na kustarehe.

Ningekwenda zangu mbali, ningetua jangwani. Selah. (Selah yamaanisha “Amina.”)

³³ Daudi, aliyependa jangwa, alipopatwa na hofu na watu hawangemwamini, nao maadui walikuwa wamemjia, alisema, “Ningekuwa na mbawa za njiwa, ningeruka hata jangwani na kukaa huko.” Ni mara ngapi nimewazia jambo lilo hilo! Laiti ningalichukua bunduki yangu ukutani, mfuko wangu wa kambi, niende jangwani ni nisirudi tena. Nimemwomba Mungu kama naweza kuishi nikaone siku hiyo. . . Sitaki kamwe ibada

ya mazishi, nilisema, “Laiti ningalienda mle mwituni mahali fulani, niegemeze huyo ‘Mweupe’ wa kale mtini. . .”

³⁴ Hiyo bunduki yangu, samahani, na—na—nasema hayo kwa ajili ya mke wangu aliyeketi pale. Mwajua, bunduki hiyo Ndugu fulani hapa alinipa miaka mingi iliyopita, niliua wanyama wakubwa hamsini na watano nayo, bila kukosa shabaha, wengine wao yadi mia saba hata mia nane. Naiita “Mweupe” kwa maana mke wangu yuna nywele za rangi nyeusi kidogo, kwa hivyo yeye alisema najali bunduki yangu kuliko ninavyomjali yeye. Lakini. . .

³⁵ Kwa hivyo, ni—ningetaka kuiegemeza mtini, na kusema, “Bwana, hebu na Joseph akaipate siku moja.” Ningetaka kuchukua mbawa za njiwa na kuruka mbali.

³⁶ Bali kama tu wakati mmoja kule juu mlimani nilipokuwa namtazama tai, na kumwona akiruka mbali (mnajua hadithi yangu juu yake), nilisema, “Ni vizuri kuwa hapa, Bwana; kama alivyosema Petro, ‘tungefanya vibanda vitatu’. Bali kule chini ya mlima walio wagonjwa na wanaoteseka wanangoja, waliopotea na wanaokufa wangoja.” Kwa hivyo hebu tufanye yale tuwezayo kungali ni mchana, na siku moja kutakuwa. . .mbawa za Tai mweupe zitashuka, Yeye atatuchukua.

³⁷ Sasa katika Mathayo 3:16, ningetaka kusoma 16 na 17:

Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akiya juu yake:

Na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyo ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye. (kwa maneno mengine, “ambaye ninapendezwa kuishi ndani yake.”)

³⁸ Sasa tunataka kunena kwa dakika chache kuhusu huyu ndege. Hua kila mara amekuwa mmoja wa ndege ninaowapenda sana. Na tukiwaza habari za hua, hua bila shaka. . .Na njiwa ni ndege walio sawa. Njiwa ni hua aliyefugwa. Wote wawili ni jamii moja. Nimeichunguza nao ni jamii moja. Njiwa na hua, wote wawili ni jamii ile ile. Tabia za ndege hawa ni za ajabu.

³⁹ Nilihubiri hapa, miaka michache iliyopita, katika mkutano wa hema hapa pamoja na Ndugu Moore, kuhusu: Mwana-Kondoo na Hua. Nadhani nyote mnaukumbuka; na jinsi kwamba hua ndiye ndege msafi sana tuliye naye, naye mwana kondoo ndiye mnyama mpole sana tuliye naye. Wote wawili ni ndege na mnyama wa dhabihu.

⁴⁰ Jinsi ilivyooneshwa vizuri hapa kwa mfano kwamba Yesu ni Mwana-Kondoo, na Mungu ni Hua. Na hua hangalitua juu ya mbwa mwitu, tabia yake si nzuri. Hangalitua juu ya mbwa, tabia yake si nzuri. Ilipaswa kuwa juu ya mwana-kondoo; tabia hizo

mbili zilipaswa kuwa sawa. Na hivyo ndivyo inavyotupasa kuwa, tabia zetu hazina budi kubadilishwa kutoka mwenye dhambi angurumaye kuwa mwana-kondoo mpole sana.

⁴¹ Na mlitambua ya kwamba Hua alimwongoza Mwana-Kondoo? Basi tazameni, Mwana-kondoo alisalimisha cho chote alichokuwa nacho kwa Hua. Na tazama ambako Hua alikomwongoza: kusulubiwa kwa ajili ya dhambi zetu sote.

⁴² Basi, Hua wa... Mungu alipotaka kuwakilisha Mwanawe, yeye alimwakilishwa kwa mnyama aliye msafi sana na mpole sana duniani, kiumbe cha duniani; bali Mungu alipojiwakilisha Mwenyewe mbinguni, ilikuwa kwa ndege aliye mpole sana na msafi sana aliye mbinguni, hua.

⁴³ Naam, hua wanahitilafiana, kuna aina nyingi zao. Kwa kawaida hua wetu ni ndege wa kijivu-jivu. Na ndipo kuna njiwa anayeomboleza, kisha kuna njiwa wa jioni. Pia kuna mwingine aitwaye hua wa sonora tuliye naye nyumbani, yeye ni ndege mdogo wa kijivu; mdogo, mdogo sana aliye na milia miekundu mbawani mwake. Kuna aina nyingi sana mbali mbali za hua, nao wanahitilafiana kwa rangi zao. Vivyo hivyo jiwa nao.

⁴⁴ Naam, hua ni hua aliyeumbwa kwa njia ya kipekee sana, kwa sababu tabia yake ni kwamba hawezi kula cho chote ambacho ni kichafu; hawezi akafanya hivyo kamwe, kwa sababu hakuumbiwa hayo.

⁴⁵ Basi, kila mara nimenena kuhusu hua akiwa mfano wa Mungu, na kunguru akiwa mfano wa mnafiki. Kunguru anaweza kukalia mzoga wa kale uliooza na kuula, siku nzima, na kuruka huko nje uwanjani na kula ngano pamoja na hua. Bali huyo hua anaweza akala ngano vizuru, bali hawezi akala mzoga uliooza. Mnaona? Hawezi akatenda hayo, hawezi kuuvumilia. Nami nalishangaa mbona yeye hangeweza kufanya hivyo; wote wawili ni jamii ya ndege, wote wawili ni ndege. Mbona hivyo? Ni maumbile yao.

⁴⁶ Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo halisi. M... Mkristo tu wa kidhehebu anaweza kupokea cho chote, bali Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili hawezi kupokea mambo ya ulimwengu. Yeye ameumbwa vingine.

⁴⁷ Niligundua ya kwamba hua hana nyongo yo yote. Hamna nyongo katika hua, kwa maana yeye hana haja nayo.

⁴⁸ Kwa hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo, yeye hana haja na uchungu wo wote, mwaona, maana yeye anaweza tu kula chakula cha Mungu. Haihitaji uchungu kukiyeusha hicho; inahitaji upendo, mwaona, ili yeye...kukiyeusha hicho chakula. Uchungu: "Lo," wao husema, "vema..." wanahitilafiana Nalo. Lakini upendo kila mara hulipokea, Neno la Mungu.

49 Naam, hana nyongo, kwa hivyo basi yeye hangeweza... hawezi kula cho chote kibaya. Na kama angalifanya hivyo, kingalimuua. Bali hamna hatari yo yote, hatakula hicho (a-haa), kwa sababu hana njaa yake.

50 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo halisi. Je, ulijua ya kwamba Mkristo halisi hana hata dhambi yo yote iliyohesabiwa kwake? Daudi alisema, "Heri mtu yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi." Unapooshwa kwa Damu ya Mwana-kondoo (si kwa kujifanya mwamini bali hasa kwa—kwa Damu ya Mwana-kondoo), Mungu hakuhesabii cho chote kilichotendwa, kwa maana uko chini ya Damu, Naye hakioni. Kuna toleo la Damu; kitu pekee anachoweza kukuona ndani yake, ni jinsi alivyokuona kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu yeye alipoweka jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo. Hiyo ndiyo tu anayoweza kutazama, kwa maana umekuombolewa kutoka kwa kila kitu ambacho kilipata kufanywa, umeoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo. Kwa hivyo hamna nyongo ndani yako, hamna tabia chafu ndani yako, kwa sababu damu ya Mwana-kondoo imetenda haya; na Mungu hawezi kukuhesabia dhambi baada ya kuwa na toleo la dhambi pale likikungoja.

51 "Vema," mnasema, "hiyo inanipa nafasi kubwa sana basi, Ndugu Branham, naweza kufanya cho chote ninachotaka." Mimi hufanya hivyo daima; kila mara. Lakini mtu awezapo kuona yale Yesu amemtendea, na akageuka na kufanya kitu dhidi yake, inaonyesha yeye hakumpokea Kristo kamwe.

52 Nina maskini mke wangu anayeketi kule nyuma. Nimempita kwa miaka kumi, naye yuna mvi kama nilivyo mimi. Sababu yake ni kwamba yeye amesimama kati yangu na—na ulimwengu wa nje. Kama ningalikuwa nikienda nchi za ng'ambo, nami... Je, hii si ingekuwa namna ya jamaa inayofaa kuishi nayo, kama ningaliikusanya jamaa yangu kunizunguka nami ningesema: "Tazama hapa, Bi. Branham, inakupasa kufahamu ya kwamba wewe ni Bi. William Branham. Usiwe na waume wengine nikiisha kuondoka. Usimkonyezee jicho mwanamume mwingine ye yote," na mambo haya yote. "Usisuhubiane kamwe. Ukifanya hivyo nitakaporudi nitakutaliki."

53 Naye angenigeukia na kusema, "Naam, mume wangu mwema, nataka kukuambia jambo fulani pia. Usimtwe mwanamke mwingine ye yote ukiisha kuondoka. Usifanye hivi na vile. Ukifanya hivyo, jihesabu tu ya kwamba umetalikiwa utakaporudi nyumbani."

54 Je, hiyo haingekuwa jamaa iliyopendana? Mwaona? La! Iwapo nampenda kweli... Ijapokuwa naamini kama ningalifanya kosa na kuteleza na kufanya mabaya, naamini angalinisamehe hilo kwa sababu yeye anipenda. Na iwapo yeye alitenda hayo, naamini ningalimsamehe hilo; bila shaka,

kwa sababu nampenda. Lakini kama nampenda hivyo, mradi tu mimi ninampenda hivyo yeye hana wasiwasi. Ijapokuwa angalinisamehe, singalimuudhi kwa cho chote kile. Ni—ni ningalijisikia mtu mwenye hatia sana ulimwenguni, singalingojea ile dakika ningalimwambia yale niliyotenda, kwa sababu nampenda. Vema, hiyo ni... Kama nampenda kwa upendo wa *phileo* hivyo, ni zaidi sana vipi upendo wangu wa *agapao* ungali kuwa kwa Yesu Kristo?

⁵⁵ Ijapokuwa ningalivuta sigara, sijafanya hivyo kamwe maishani mwangu; bali hata kama ningalifanya hivyo, Yeye angalinisamehe, naamini Yeye angenisamehe. Kama ningelewa pombe, sijawahi maishani mwangu, lakini naamini angenisamehe hilo. Nami nampenda kupita kiasi, (Mungu, unisaidie,) sitaki kufanya kitu kama hicho; mwaona, kwa maana nampenda. Upuzi huo umeniondokea mimi, kwa sababu aliponigeuza kutoka kwa kunguru nikawa hua nilibadilika, tamaa ya mambo hayo na kadhalika ziliniacha; basi sihesabiwi dhambi kwa sababu sikusudii kuitenda, sina shauku ya kuitenda.

⁵⁶ Sasa jambo jingine kuu juu ya huyu hua. Yeye ni ndege wa ajabu. Je, umepata kuwaona ndege wote...

⁵⁷ Mmoja wa ndege niwapendao sana ni robin. Naam, enyi vijana acheni kumuua robin wangu, mwaona, kwa sababu siwatakeni kufanya hivyo. Robin wangu, mwajua alivyopata kifua chake chekundu? Mwajua, siku moja Mtu mmoja alikuwa akifa msalabani, hamna mtu angalimsaidia, Mungu alikuwa amemwacha Mtu huyo, naye alikuwa yuafa. Mikono Yake ilikuwa ina misumari, miguu Yale na mbavu Zake zilitoka damu, taji kichwani Mwake ana miiba, damu ikitiririka usoni Mwake. Na kulikuweco ndege mmoja aliyepita hapo, ndege mdogo, mwenye rangi ya hudhurungi. Naye akatazama hayo, alikuwa... akaona kwamba yalikuwa msiba mkuu sana aliopata kuona. Naye alijua alikuwa tu ndege mdogo, lakini akaitazama hiyo misumari mikubwa mno na mikatili ya Kirumi iliyopigiliwa mkononi Mwake, naye akaruka huko na kwa mdomo wake mdogo akajaribu kuing'oa. Kifua chake chote kikalowa damu, tangu wakati huo kimekuwa chekundu. Nataka kifua changu kifunikwe na Damu Yake, pia, nikimtetea nitakapokutana naye. Nampenda maskini robin.

⁵⁸ Lakini, mwajua, maskini robin inambidi kuoga; bali mwajua, hua haimbidi kuoga; la. Yeye ana aina fulani ya mafuta ndani yake ambayo humpaka mafuta na kumweka akiwa msafi kutoka ndani hata nje. Mnajua hivyo? Hua anayo! Hua hujipaka mafuta. Je, umewahi kumchukua mmoja ukanukia harufu hiyo yake, njiwa ama cho chote kile? Hayo ni mafuta yanayotoka ndani yake. Mwili wake hutengeneza kifuko cha mafuta ambapo huhifadhi manyoya yake yakiwa masafi daima upande wa nje

kwa sababu yeye ni msafi toka ndani hata nje. Hiyo ni kweli. Yeye ni ndege mdogo wa ajabu sana.

⁵⁹ Naam, najua mnaweza kuwawinda hapa, nafikiri; katika Louisiana. Msifanye hivyo! Jamani, singalitenda hilo. Nakisia ningalikuwa na njaa, ingekuwa sawa, bali si—singalimpiga bunduki ye yote kwa vyo vyote.

⁶⁰ Kuna... Hua ana jambo kuu na la kigeni katika jamaa yetu. Siku moja wakati nyanya yangu... Anatoka humu Kentucky, kutoka kijiji cha Cherokee. Alikuwa yuafa, maskini mwanamke huyo, naye alikuwa... Wao walikuwa... Nafikiri wanauita ugojwa wa kuvimba matezi ya shingoni au cho chote kile, alikuwa akifa. Naye babu yangu akapiga magoti kandoni mwa kitanda; huku mama, Shangazi Birtie, Shangazi Howlie, wote wakapiga magoti kuzunguka kile kitanda; Mjomba Charlie, mvulana mdogo, wa miaka minne) mtoto mchanga; mama, wa kwanza, akiwa ana yapata umri wa miaka kumi na miwili. Naye alikuwa amechanulia nywele zake nyeusi kitandani, na akaanza kuimba, "*Mwamba wenye Imara, kwako nitajificha*," alipokuwa akifa. Babu yangu, wakati huo, hakuwa Mkristo. Nilimbatiza akiwa ana umri wa miaka themanini na saba, katika Jina la Yesu Kristo, upande wa chini wa mto hapa ambapo Malaika wa Bwana alitokea.

⁶¹ Lakini alipokuwa akiimba wimbo huu, huku mikono yake midhaifu imeinuliwa juu hewani, hua akaingia mlangoni; akaja na kuketi juu ya kitanda, akaanza kunong'ona kwa sauti nyororo. Mungu akaitwaa nafsi yake.

⁶² Nilienda huko London, Uingereza pamoja na Ndugu Jack na Ndugu Gordon Lindsay, na kulikuweco mwanamke jina lake Florence Nightingale (anadai kuwa, nafikiri, kitukuu ama cho chote kile cha hayati Florence Nightingale) ambaye aliniandikia barua nyingi. Alikuwa kule Afrika kusini, akifa kwa kansa. Naye alikuwa na picha; mmeiona kwenye kitabu. Sijamwona binadamu kama huyo maishani mwangu. Ndugu Jack, naamini, alikuwa pamoja nami siku hiyo. Tukaenda katika nyumba ya muhudumu, nyumba ya kasisi, nyuma tu ya kanisa ambamo walikuwa wamemleta.

⁶³ Tulipokuwa tungali kule... ambako ndege ilitua, wakaita majina yetu, naye alikuwa katika gari la kuchukulia wagonjwa hapo wakati huo; alikuwa amerushwa kwa ndege kutoka-kutoka kule Afrika kusini, akijua ya kwamba nilikuwa naja Uingereza wakati huo. Mhudumu akampeleka katika nyumba ya kasisi, kwa hivyo tukaenda kule kumwombea.

⁶⁴ Nimewaona watu wengi sana walio wagonjwa, lakini mikono yake midogo haikuonekana yenye upana unaozidi inchi moja, fu—fuvu lake la kichwa mahali lilipounganishwa, ungeweza kupaona. Naye... viungo vyake humu juu kabisa karibu na kiweo chake havikupita hivi, yapata inchi mbili kutoka upande

mmoja hata mwingine, mfupa tu. Naye hangaliinua mikono yake, alikuwa mnyonge sana kuinua mikono yake. Naye alikuwa akijaribu kusema kitu, nami sikumsikia vizuri. Na hatimaye nilipomsikia, naamini kupitia kwa mwuguzi, yeye alisema, “Ndugu Branham, omba ya kwamba Mungu ataniachilia nife.” Hangeweza... hakutaka kuishi. Nami nikaona, na majoji yalikuwa yakitiririka upande mmoja wa mifupa ya usoni. Alikopata unyevu wa kutosha ndani yake kulia, sijui mimi; kwa maana mishipa yake ilikuwa imebonyea, naye alikuwa katika bali mbaya sana. Kwa kuwa nilikuwa nimekuja kuwaombea wagonjwa, singalimwombea afe. Lakini alionekana tu kama hangalikufa, aliendelea tu kuishi.

⁶⁵ Nami nikapiga magoti pamoja na mchungaji wenu, chumbani kuomba. Na nilipopiga magoti kuomba, hua mdogo akaruka dirishani; akaaza kunong'oneza kwa sauti nyororo. Nilipomaliza kuomba, nikafikiri alikuwa hua aliyefugwa pale mahali fulani. Nje kulikuwa na ukungu, jinsi Uingereza ilivyo, viziwa vya Uingereza mle. Na huyu hua mdogo akaacha kunong'oneza na akaruka akaenda. Nikaondoka nikaweka mikono yangu juu yake na kuliitia jina la Bwana. Na yule mwanamke ni bibi mkubwa mno na mwenye nguvu na afya siku hizi juu ya mbawa za Hua.

⁶⁶ Yeye hujiweka safi kutoka upande wa ndani. Mkristo hufanya hivyo pia, yeye hujisafisha kutoka ndani. Hiyo huondoa maovu... Hahitaji nyongo yo yote kuyeyusha cho chote, kwa maana yeye hali hicho. Mnaona? Yeye ni msafi kutoka ndani hata nje.

⁶⁷ Sasa twaona ya kwamba ndege huyu... Nina mambo mengi niliyoandika hapa, lakini saa ingali inazunguka. Huyu ndege alitumiwa pia katika Agano la Kale kwa sadaka, kwa upatanisho na kwa utakaso. Hebu tutaje kwa moja katika mwanzo 15:9. Hebu tukitafakari kifungu hiki kwa muda mchache tu. Sasa Ibrahimu alikuwa... alimuuliza Mungu hapa, angefanyaje hili. Naye Mungu analitimiza Neno Lake kwa Ibrahimu, naye anafanya hivyo kwa njia ya ajabu. Tuanzie yapata... Tuanzie kifungu cha kwanza, sitaki kuharakisha hili.

Baada ya mambo haya Neno la Bwana BWANA likamjia Abramam katika njozi... (mwaona, Ibrahimu alikuwa nabii, kwa hivyo aliona maono)... Usiogope Ibrahimu: Mimi ni ngao yako, na thawabu... kubwa sana, (Yehova-nissi, mwaona.)

Ibrahimu akasema, Ee... akasema, Bwana MUNGU... (tazama herufi kubwa B, BWANA Mungu.” Elohim! Mwaona?)... Bwana Mungu... (Katika... utanipa nini, nami naenda zangu hali sina mtoto, na anayemiliki nyumba yangu ni huyu Eliezeri, Mdamaski?)

Abramu akasema, Tazama, hukunipa uzao, na mtu aliyezaliwa nyumbani mwangu ndiye mrithi wangu. Nalo neno la BWANA likamjia likinena, Huyu hatakurithi... (alikuwisha kumpa ahadi, mwajua. Si... mwaona, papo hapo Ibrahimu angalishindwa, bali hiyo ahadi haina masharti; hilo agano, halina masharti)... bali atakayetoka kwa viuno vyako ndiye atakayekurithi. (naye yuna umri wa miaka mia moja sasa) Akamleta nje, akasema, Tazama sasa mbinguni, kazihesabu nyota kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako. (mtu asiye na mtoto, na sasa yuna umri wa miaka mia moja.)

Akamwamimi BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.

Kisha akamwambia, mimi ni BWANA niliyekuleta kutoka Uru wa wakaldayo nikupe nchi hii ili uirithi.

Akasema, Ee Bwana MUNGU...ama Bwana... nipateje kujua ya kwamba nitairithi?

68 Sasa sikiza hili:

Akamwambia, unipe ndama wa miaka mitatu, na mbuzi mke wa miaka mitatu (watazame hao watatu sasa, “wa miaka mitatu”)...na kondoo mume wa miaka mitatu, na hua, na mwana njiwa. (wote wawili ni watu wale wale, vyote viwili ni vitu vile vile. Mnaona, alitumiwa kwa sadaka ambayo ilimwonyesha Yesu Kristo kimbele)

69 Angano lile lile lilifanywa. Mwajua, jinsi alivyowapasua, na jinsi hii... .

70 Ama zile nyakati za kale, walipotwaa... walipofanya agano, wangelichukua na kuandika ma—mapatano. Nao wangemuua mnyama, wakasimama katikati yake; wapasua hiyo ahadi vipande viwili, mtu mmoja akachukua kipande kimoja... .

71 Kama dobi wa Kichina alivyokuwa akifanya. Mchina hapa, hangaliandika Kiingereza, kwa hivyo akaandika pale na kupasua kipande cha karatasi na kukupa sehemu yake. Nanyi mwa—mwakumbuka dobi wa Kichina walipokua wakifanya hivyo. Nawe...sehemu hizo zao mbili ilizibidi kulingania, kusudi upate nguo zako. Unaona, haungalim danganya, kwa sababu alikuwa na ile sehemu nyingine yake. Ungeweza kuandika jina lako, bali haungalipasua hiyo karatasi tena ikalingane. Waona? Kwa hivyo, ilimpasa... ilibidi kiwe kipande kile kile cha karatasi.

72 Kwa hivyo hivyo ndivyo walivyofanya katika zamani za Kimashariki, zamani...ama zamani za kale katika siku za Kimashariki. Wao wangemuua mnyama, wasimame kati yake, wapasue kipande cha ngozi ya mbuzi, mmoja akakichukua

kimoja . . . Na ahadi ilipoyakinishwa, wakaviunganisha vipande hivyo pamoja navyo vilipaswa kuumana kwa ndimi kikamilifu.

⁷³ Sasa, lile Mungu analomwonyesha hapa ni hili, juu ya hizi sadaka, zinanena juu ya Kristo; jinsi Mungu alivyompeleka Yesu Kalvari na kumpasua vipande, na kuupokea huo mwili mbinguni na kumtuma Roho juu yetu, na Roho yule yule aliyekuwa juu Yake hana budi kuwa juu yako upate kuungana na huo Mwili, upate kuwa Bibi-arusi wakati wa mwisho. Mwaona? Mwaona? Hiyo ni kweli. Mnaona? Haitakuwa dhehebu, sasa. Itakuwa Neno, jinsi alivyokuwa. Mwaona?

⁷⁴ Kama vile hilo Neno halina budi kuja kwa Neno, kama chembechembe katika mwanadamu. Unajua, mwi—mwili wako unapojengwa, si chembechembe moja ya mwanadamu, halafu ya mbwa, ndiposa ya nguruwe. Jamani, la, la. Wote ni chembechembe ya binadamu. Hivyo ndivyo Mwili wa Kristo ulivyo, wote ni Neno la Mungu. Si sehemu Yake tu, mapokeo yakaongezwa Kwake; la *wote* ni Mwili wa Kristo.

⁷⁵ Sasa, tunaona hapa ya kwamba alitumia hua na kindi la njiwa, kwa sababu wote ni wa jamii ile ile. Naam, kila mara ninyi. . .

⁷⁶ Kwa hivyo tazama (nitataja tu baadhi ya haya Maandiko) Mambao ya walawi 12, na kifungu cha 6. Tunaona hapa taratibu ya kutakaswa kwa mwanamke; kama mwanamke alizaa mtoto, ilimbidi kungoja. Ikiwa alikuwa mvulana, ilimbidi angoje siku thelathini na tatu kabla hajaingia kwenye kusanyiko pamoja na hua, kwa ajili ya utakaso. Kama alizaa msichana, ilimpasa kungoja siku tisini na sita kabla hajaingia kwenye kusanyiko.

⁷⁷ Sasa twaona hapa, katika kifungu cha 6:

Kisha hizo siku za kutakaswa kwake zitakapotimia, kwa ajili ya mwana, au kwa ajili ya binti, ataleta mwana-kondoo wa mwaka mmoja kuwa sadaka ya kuteketezwa na kindi la njiwa, au hua, kuwa sadaka ya dhambi, awalete mlangoni pa hema ya kukutania, na kumpa kuhani;

⁷⁸ Mwaona, hawezi kuingia bado kwa sababu siku zake, hazijakwisha bado, bali anaweza kumpa hizi-kuhani mlangoni, kwa ajili ya sadaka yake. Mnaona, hua au kindi la njiwa. Wote wawili ni jamii moja.

⁷⁹ Sasa—sasa alitumiwa kwa upatanisho na kwa upatanisho wa dhambi, hua mmoja. Ama kwa ukoma ambao ni mfano wa dhambi ulileta hua wawili: kichwa cha mmoja kilikatwa, akainamishwa juu chini na kunyunyiziwa huyo mwingine; kisha huyo mwingine akaachiliwa huru. Na huyo hua aliporuka, akaiosha ardhi kwa damu ya mwenziwe, na hiyo damu ikamlilia Mungu, “Mtakatifu! Mtakatifu! Mtakatifu ni Bwana Mungu!”

⁸⁰ Hamwezi kumwona mwenzi wetu Yesu Kristo anayekufa? Yeye aliuaa na kunyunyiziwa juu yetu, tupate kuwa huru, tukipaza sauti “Mtakatifu! Mtakatifu!” kwa Bwana. Ni mifano mizuri vipi. Laiti ningalikuwa na sauti.

⁸¹ Sasa ni mfano wa Roho Mtakatifu aliye mkuu kama tulivyosoma katika Ufunuo 3:16; alitumiwa na Mungu kwa ishara, huyu hua.

⁸² Nuhu alipewa ishara, kama vile ndugu amekwisha kuimba habari zake. Mungu alikuwa na ghadhabu, na hakuna cho chote kingezuia hasira Yake, kwa maana alisema, “Siku utakapokula hayo, siku hiyo utakufa.” Naye Nuhu aliishapata neema machoni pa Mungu na kujenga safina kulingana na mijengo... yale maagizo, namaanisha, ambayo alikuwa amempa. Naye akaelea.

⁸³ Naweza kuwaza... yaliyotendeka siku hizo wao waliposema, “Mzee huyu kule juu kilimani, mzee mshupavu wa dini, akijenga safina, akisema, ‘itanyesha’, na haijanyesha kamwe.” Bali... .

⁸⁴ Nuhu akasema, “Itanyesha kwa vyo vyote.”

⁸⁵ Ndiposa najua siku aliyolingia, nafikiri ya kwamba... siwezi kukumbuka ilikuwa siku gani, naamini mei kumi na saba. Nuhu akaingia safinani, naye Mungu akafunga mlango.

⁸⁶ Na mawingu yakaanza kuja, na mvua ikaanza kunyesha, mifereji ya maji machafu ikaanza kujaa, chemchemi za vilindi zikafunguka, visima vikabubujisha maji yao. Mwishowe watu wakaingia nyumbani mwao, wakapanda juu. Ile safina ya kale ikakaa papo hapo vivyo hivyo.

⁸⁷ Muda si muda wakati maji ya kutosha yaliizunguka, ikaanza kuinuliwa juu zaidi na zaidi. Hao watu wakipiga milango na kulia kwa sauti kuu, bali hai—haikuwafaidi kitu, Nuhu hangaliufunga mlango. Mungu aliufunga, Mungu ndiye pekee awezaye kuufungua.

⁸⁸ Ndivyo ilivyo kwenye Safina yetu, Yesu Kristo; Mungu alitufungulia mlango kule Kalvari, Yeye ataufunga bila shaka tu kama alivyoufungua.

⁸⁹ Nayo ikaelea, zaidi na zaidi, huenda ikawa kina cha maili moja juu ya uso wa dunia wakati dunia hii ilikuwa ikitapatapa kutoka kwa... kutoka kwa mzunguko wake wa kawaida. Nayo safina ikazunguka na kuzunguka, na kwenye vipande vikubwa vya vitu na miti, na juu ya milima na kadhalika, ikienda mrama siku arobaini mchana na usiku.

⁹⁰ Na pepo zilipoanza kutulia... .

⁹¹ Hasira ya Mungu ni ya kutisha. Upendo Wake ni Mtakatifu na wa kiungu; na hasira Yake ni ya kiungu tu—ya kiungu tu kama upendo Wake ulivyo, kwa sababu Yeye hana budi kuhukumu kwa sababu Yeye ni hakimu. Yeye ni mtoa sheria, na sheria bila adhabu si sheria. Kwa hivyo hapana budi kuwe na

adhabu ya sheria. Na unapovunja sheria za Mungu, hapo ndipo unapoadhibiwa.

⁹² Sasa twaona ya kwamba baada ya Nuhu kuelea kule, bila shaka mwenye ugonjwa wa baharini kwa sababu ya kunguruma huko kote na vishindo, na hasira ya Mungu ikipondaponda na kubana, na vilio na kadhalika. Ndipo ikaanza kutulia, hamna kitu kilichotendeka. Siku zikapita, hamna kilichotendeka. Labda akiba ya chakula cha wanyama na kadhalika ilikuwa ikipungua, hamna kilichotendeka. Kwa hivyo akawaza, “Nashangaa . . . siwezi kuona nje.”

⁹³ Safina ilijengwa hivi kwamba (mara ulipoingia ndani), kulikuweco dirisha moja tu ndani yake, nayo ilikuwa juu kabisa. Haungaliangalia upande, haungaliangalia upande wo wote ila moja kwa moja juu. Na hivyo ndivyo Safina, Yesu Kristo, alivyo. Hauwezi kumwalia mtu anayefuata, hauwezi kutazama cho chote ila Kristo unapokuwa katika hiyo Safina kwa sababu kuna mlango mmoja tu, naye ndiye huo mlango tulionena habari zake asubuhi ya leo. Inakupasa uzidi kutazama juu, “Kwa sababu atakayetia mkono wake kulima, kisha akageuka akaangalia nyuma, hafai kwa kulima.”

⁹⁴ Sasa, kama ilivyo katika safina hii . . . Naye angalionu na labda nuru ya jua, bali alishangaa alikuwa wapi. Safina ilikuwa ingali inaelea, angalisikia mawimbi yakipiga kuta zake, bali alijua siku nyingi ziliisha pita, bila shaka maji yalikuwa yanapungua wakati huo. Kwa hivyo akaenda akampata ndege asiye mwaminifu, mhaini, na akamjaribu, na kumtuma nje. Alikuwa kunguru, na kunguru huyo hakurudi kamwe, kwa sababu alipata anasa kule nje, nje ya safina ya Mungu. Aliruka toka kwa mzoga mmoja hata mwingine, akila mizoga na nyama zilizoza ambazo zilielea majini; naye aliridhika kabisa.

⁹⁵ Kwa hivyo baada ya siku kadhaa akajaribu tena, kwa kuwa alijua . . . Yeye hakutaka kutoka nje kwenye hasira ya Mungu. Kwa hivyo akamwachilia hua. Na huyu hua alikuwa na tabia tofauti na yule . . . Hakuwa mwewe, wala anayekula vilivyooza, yeye hula tu vitu visafina halisi. Naye alikuwa ameridhika kabisa kwa sababu hangepata cho chote cha kuwekelea nyayo za miguu yake, akarudi safinani. Nuhu akasema, “Vema, gharika ingaliko.”

⁹⁶ Kisha akangoja siku kadha zingine, naye akatumana tena, kama ombi lake, “Ee Mungu, hasira yako imetulizwa? I—imekwisha ghadhabu Yako, Bwana? Yote imemalizika?” Naye akasema, “Naam, nikimtuma sasa, huenda akakaa kule iwapo gharika imepunguka, huenda akakaa.” Bali akamtuma kwa maombi, na ndipo alipokwenda huko akiongozwa na Mungu, akachuna jani la mzeituni toka kwa mti, na akarudi na kipigapiga ndirishani kwa mdomo wake tena.

⁹⁷ Mungu alimtumia hua kwa ishara. Alirudi akisema ya kwamba “gharika imekwisha,” ndiposa Mungu akafungua mlango, nao wakatoka. Hiyo ni Mwanzo 8:8.

⁹⁸ Pia alitumiwa katika Mathayo 3:16 tena wakati hasira ya Mungu alikuwa duniani. Na hapakuwepo njia, usiku wenye giza sana, usiku wa manane, makanisa yalikuwa yamepotosha mambo sana hata hapakuwepo njia ya kuepukia. Na kulikuweko walimu wa uongo, kuzuka kwa mambo ya kila namna, maungamo ya kila namna yakiinuka, lakini Mungu akamtumia hua tena. Ilimpendeza, Mwanawe Yesu alimpendeza Yeye sana, hata akamtambulisha.

⁹⁹ Naam, wao hawangaliamini ya kwamba huyu mtoto mchanga aliyezaliwa mle zizini katika hori la majani makavu. . . kabla baba yake na mama yake, walivyodhaniwa kuwa, hawajaona. hawangaliwazia Mungu akitumia kitu kama hicho. Kwa hivyo ilimpasa kutambulishwa kwa ulimwengu; na siku hiyo kule chini mtoni, aliposhuka kule kujithibitisha kuwa kazi Bora ya Mungu (ambayo nilinena habari zake asubuhi hii). . . Alipokuwa mtiiifu kuingia majini. . .

¹⁰⁰ Sasa ukichuguza pale, kuna somo kubwa. Yohana alikuwa mtu mkuu sana ulimwenguni, wakati huo. Yesu alisema, “Hajaondokea mtu kamwe aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama yeye,” hadi wakati huo. Naye alikuwa nabii. Mnaamini hilo? Sasa, kumbuka, kama Neno la Mungu litakuja kwa cho chote nchini, itakuwa nabii. Hiyo ndiyo njia ya Mungu daima. Je, mnaamini ya kwamba Yesu alikuwa Neno lililodhihirishwa katika mwili? Kwa hivyo kuna njia moja tu Yeye anayoweza kuja kujulishwa; si na makuhani.

¹⁰¹ Yeye hakuenda kule na kusema, “Kaiyafa, je, utanijulisha? Kama angalifanya hivyo, angelifanya kosa lile lile Daudi alilofanya katika somo letu hivi majuzi; mwaona, kama angalienda kanisani na kusema, “Je, utanijulisha Mimi?”

¹⁰² Chunguza tu Yeye alipozaliwa, hata hivyo. Alipozaliwa, Yeye alizaliwa katika kivuli cha kanisa. Na huenda ikawa walikuwa wakipiga kengele na kila kitu, bali ni wachungaji waliomtambua, na mamajuzi. Mwaona?

¹⁰³ Na ndiye Huyu hapa sasa juu. . . tayari kwa huduma Yake. Na iwapo yeye ni Neno. . .

¹⁰⁴ Kulingana na mpango mkuu wa Mungu, Neno linaweza tu. . . “Bwana Mungu hafanyi neno lo lote hata kwanza awafunulie watumishi Wake manabii.” Huo ndio mtindo Wake daima, hapana budi iwe hivyo; wakati zile mihuri zilipofunguliwa, wakati kila kitu kinginecho. Tukio lo lote kubwa linapotendeka duniani, Mungu hulifunulia manabii Wake.

¹⁰⁵ Na Yohana alikuwa nabii, kwa maana alikuwa akitabiri “Yeye angekuja.”

¹⁰⁶ Kisha kule chini kandoni mwa kilima siku moja... wakati mahojiano yalikuwa yakiendelea, kundi la makuhani wakisimama huko. Nao wakasema, “Wataka kuniambia ya kwamba unajiita nabii, na kusimama mle kwenye hayo matope?” (si kanisani, kwa sababu hawengemkubali) “Unasimama humo matopeni, na kuniambia ya kwamba wakati unakuja ambapo Yehova aliye mkuu aliyeagiza sadaka hizi, ambapo Yehova aliye mkuu aliyejenga hili hekalu, aliyeingia humo kama Nguzo ya moto, ‘Siku inakuja ambapo sadaka hiyo ya kuteketezwa ya kila siku itakapoondolewa.’?”

¹⁰⁷ Yeye akasema, “Atakuja Mtu fulani, Naye yu miongoni mwenu sasa (mahali fulani kule nje,) naye ataondoa dhambi.” Kuhani alichukizwa naye.

¹⁰⁸ Yohana akainua macho yake juu! Naam, yeye ni nini? Nabii! Nalo Neno ndilo hili, Neno likaja moja kwa moja kwa huyo nabii, likaingia majini. Yohana akasema, “Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Huyu hapo, ndiye Huyo.” Yesu hakusema neno kamwe, akaingia moja kwa moja majini. Nami naweza kuona pale, akisimama majini (waza kuhusu mchezo wa kuigiza), watu wawili walio wakuu sana waliowahi kuja duniani: Mungu Neno, na nabii Wake.

¹⁰⁹ Tazama, Neno limekwisha kuja kwa nabii katika wakati huu wa neema, majini (a—haa). Nilifikiri mngeipata (a—haa). Majini! Ufunuo wa kwanza wa Neno ulikuwa majini. Sasa mwaona ambapo Bibi-Arushi alipoanzia, ujumbe wa Nuru ya Jioni? Majini! Lile Neno, Neno la kweli lisilochanganyikana na kanuni za imani, bali lililokuja kwa nabii majini, kwa maji.

¹¹⁰ Tazama, ungewaza macho ya Neno na macho ya nabii yakikutana majini? Jamani, hiyo imezidi sana kwangu. Ndiye huyo nabii amesimama pale, ndiye huyo Neno amesimama pale, wakitazamana uso kwa uso. Naye nabii akasema, “Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe, mbona Waja kwangu?”

¹¹¹ Naye Neno akasema . . . Haina budi kuwa kweli.

Basi hebu niwaonyeshe mchezo wa kuigiza hapa:

¹¹² “Yohana, wewe u nabii, unajua Neno.” Mwaona? “Unanitambua mimi, unajua mimi ni nani.”

¹¹³ “Mimi nahitaji kubatizwa na Wewe,” Yohana akasema.

¹¹⁴ Yesu alisema, “Kubali hivi sasa. Hiyo ni kweli kabisa, wewe unahitaji kubatizwa Nami. Bali kumbuka, Yohana, ukiwa nabii, ndivyo itupasavyo, au ni wajibu wetu (kama Neno *na* nabii), kutimiza kila Neno (a—haa). Kwa kuwa, Yohana,” (ufunuo ndio huu sasa) “Yohana, unajua Mimi ni Nani, Mimi Ndimi ile Sadaka. Na kulingana na Neno la Mungu, sadaka ilipaswa kuosha kabla haijatolewa kama sadaka.” Sivyo? Neno... “Mwana-kondoo alioshwa ndiposa akatolewa kwa sadaka, Nami ndiye huyo Mwana-Kondoo. Nami sina budi kuoshwa kabla

sijatolewa kwa ulimwengu kwa ajili ya sadaka. Kubali hivi sasa, Yohana, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kama Neno na nabii pamoja.”

¹¹⁵ Vema, hapawezi kuwa na kosa. Sasa kila moja ya mambo haya . . .

¹¹⁶ Naam, mwaona, kama si mpango uo huo, Yohana angalikuwa kama ye yote wetu; kwa hivyo wao husema, “Naam, na—najua wewe u nani, Bwana.”

¹¹⁷ “Vema,” Yeye akasema, “ngoja kidogo, mimi ni Neno (a—haa). ‘Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa *kila* Neno. Hawa aliacha moja (a—haa), lakini inakubidi kuchukua *kila* Neno. Nami ndiye hiyo sadaka, na sina budi kuoshwa kabla sijatolewa. Bali uliyosema, Yohana, ni kweli.”

¹¹⁸ Yohana akiwa nabii, akijua ilipasa Neno litimizwe, yeye alikubali hivyo na akambatiza. Na alipotoka majini, kukaja ujumbe toka mbinguni juu ya mbawa za Hua, “Huyu ni mwanangu, mpendwa Wangu.” Yeye alituma Ujumbe wa ukombozi wa neema kwa mbawa za Hua, akaja akiruka chini kutoka mbinguni. “Duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.” Sadaka ilikuwa tayari papo hapo; alikuwa amekuzwa, akalishwa, huduma Yake ilikuwa tayari, Neno ambalo lingekomboza ulimwengu mzima, “Imekwisha?”

¹¹⁹ Hua ametumiwa katika Biblia kama mfano wa amani, na pia anatumiwa na mataifa kama mfano wa amani. Tuna mataifa . . . Taifa letu limewakilishwa na tai. Na kuna ndege wengine wa mataifa mengine, Rumi ina tai, Ujerumani ina tai; mengi yao, ndege wakuu wa angani. Bali katika hayo yote, hua huonyesha mfano wa amani katika mataifa yote. Ni jambo la ulimwengu mzima.

¹²⁰ Kama Ndugu Green alivyosema usiku mmoja, Ndugu Pearry Green alisema, “Ishara ya kujisalimisha ni ‘inua mkono wako.’ Katika taifa lo lote, kuinua mkono wako, ni kujisalimisha.” Akasema, “Mnapoimba, mkiinua mikono yenu, mnatoa yote.”

¹²¹ Na hua ni mfano wa amani katika kila taifa. Mbona amefanywa kuwa hivyo? Kwa sababu ya upole wake, na kwa sababu ya kutokuwa na udhia. Hiyo ndiyo sababu yeye ni mfano wa amani.

¹²² Jambo jingine kuhusu hua, yeye ni ndege mpenda nyumbani. Hupenda kukaa nyumbani.

¹²³ Jambo jingine kwake, ni mwaminifu daima kwa mwenzi wake. Hua, wa kiume au wa kike, hawaachani. Huyu wa kike humpata mwenzi wake wakati wa kutaga. Mnaona, hiyo inastahi uumbaji mkuu wa Mungu. Hiyo ndiyo sababu Yeye alimfanya Hawa kitu kilichotoka kwa kingine. Mwaona? Kama angaliumbwa kama jike wengine, wakati wake ulipofika wa kupata mimba, angalimpata mwenziwe; bali angefanya hivyo

wakati wo wote. Mwaona? Na hiyo ndiyo njia, hivyo ndivyo ilivyo. Ni. . . Hatutaki kuingilia hilo, kwa sababu ninayo katika *Ndoa na Talaka* na kadhalika. Na jinsi. . . Lakini, yeye ni wa kuheshimiwa na ameletewa huo uadilifu, na mnajua jinsi nilivyohubiri juu yake usiku uliopita. Vema, tazama, yeye yuna wajibu mkubwa.

¹²⁴ Lakini hua daima ni mwaminifu kwa mwenziwe. Hamwachi kamwe.

¹²⁵ Na hebu nikome hapa kwa kitambo kidogo tu niseme hili. Bibi-Arasi wa kweli, hua wa kike, ni mwaminifu kwa mwenziwe, pia. Hataingiza fundisho lo lote la sharti, mafundisho yo yote ya kidhehebu, cho chote cha kilimwengu. Atadumu akiwa mwaminifu kwa mwenziwe, Neno; mwaminifu daima.

¹²⁶ Na kwa tabia hii ya kupenda nyumbani, kwa matendo yake ya upendo wa nyumbani, ametumiwa kwa ufanisi kama njiwa mbebaji. Kwa sababu anapenda nyumbani, mwachilie mahali po pote, kila mara atarudi nyumbani. Atarudi nyumbani.

¹²⁷ Tungetaka kusesitiza hilo kwa kitambo kidogo, nanyi Wakristo mtafahamu ninayomaanisha. Kila mara atarudi nyumbani, kwa hivyo basi ametumiwa kama njiwa mbebaji. Anatumia wakati wa vita, ilikuwa hivyo; wangali wanawatumia, njiwa wabebaji kubeba ujumbe. Kwa hivyo mwaona basi, hiyo inamfanya hua, kwa Mungu na mwanadamu pia, mjumbe; hua ni mjumbe. Alikuwa mjumbe kwa Nuhu, kumwambia Nuhu ya kwamba “kuna amani tena.” Alitumiwa na Mungu kuthibitisha ya kwamba huyo alikuwa Mwanawe, “Ile Sadaka ya kuleta amani juu ya dunia kwa watu aliowaridhia.” Alitumiwa kama mjumbe.

¹²⁸ Papa hapa nina hadithi dogo akilini mwangu, niliisoma wakati mmoja katika kitabu fulani. Naam, sitaki kusema hii ni kweli, huenda iko katika *Mwisho wa Vita vya Kwanza vya Dunia*. Sina hakika ya hilo sasa; mkikosa kuiona basi nimekosea. Au nilisoma katika kitabu fulani. . . ni miaka mingi iliyopita. Bali bila shaka ilikuwa ni—ni. . . kusema kweli ni—ni jambo la ajabu lililotendeka.

¹²⁹ Askari wa Kiamerika walikuwa wamenaswa na mishindo ya bom-bomu za Kijerumani, nao walikuwa katika kitu kama shimo. Ninyi askari, nakisia, mnafahamu jinsi walivyokuwa katika upelelezi mahali fulani. Nao wakanaswa, nao walikuwa tu na risasi chache tu zilizobakia. Na Wajerumani walikuwa wakisonga mbele katika vikosi vikubwa, wakija kutoka kila mahali. Nao walijua ya kwamba wasipopata msaada wa kijeshi, msaada mdogo, wangekufa wote punde tu; (iliwabidi kufa) huku Wajerumani wakishuka moja kwa moja mlimani, wakitazama shingo zao, wakiwaendea moja kwa moja hivyo.

¹³⁰ Na mmoja wao akakumbuka ya kwamba alikuwa na hirizi ndogo, njiwa mdogo. Kwa hivyo alijua ya kwamba huyu njiwa,

kama angalitoka pale, angalipeleka ujumbe kwa makao makuu ya hicho kituo chao. Na kwa hivyo wao wakaketi chini na kuandika kijibarua, “Tumenaswa mahali *fulani* katika sehemu *fulani*. Tumeishiwa na risasi, katika masaa machache itatubidi kujisalimisha, la sivyo, tutauawa ovyo ovyo.” Nao walikifungilia hiki kwa pini, au wakakifungilia m—mguuni mwa huyu hua mdogo na kumwachilia.

¹³¹ Basi, yeye ni ndege mpenda nyumbani, kwa hivyo... Anafanyaje? Anarudi nyumbani kwa ajili ya...kukutana, kupata mwenziwe. Alifadhaishwa naye, ingempasa kurudi nyumbani.

¹³² Na aliporuka juu, Wajerumani waliona yaliyotendeka. Kwa hivyo walivyofanya, wakaanza kumpiga risasi huyo njiwa. Na mmoja wao akampiga kwa bom-bomu kipimo cha .30 au risasi, ikavunja mguu wake. Nyingine ikapasua kipande kikumbwa mgongoni mwake. Kifua chake kilichubuliwa kutoka upande hadi mwingine. Moja ya mbawa zake ikavunjwa, ncha yake ikavunjiliwa mbali, naye akaruka kwa upande. Bali akazidi kupaa juu, na mwishowe akafaulu. Huku amelemazwa; akajeruhiwa, akavunjwa, akachubuliwa, bali alianguka mle kambini akiwa na ule ujumbe. Huyu alikuwa hua mkuu.

¹³³ Ila, lo, ndugu, Isaya 53 inatuambia juu ya Mmoja, kashuka kutoka Nyumbani akiwa na yote yaliyokuwa mema:

Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu, Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.

¹³⁴ Magonjwa, ushirikina, na mashetani yalikuwa yametunasa, hakukuwa njia ya kuepukia, kanisa lilikuwa limekosea, walikuwa wameenda kombo kwa mambo ya kidhehebu (na Mafarisayo, Masadukayo, na kutakaswa kwa vyungu na sufuria), na Neno la Mungu likatanguka. Lakini maskini Hua huyu kashuka, na kuna jambo moja tu lingalitendeka: ilipaswa kuwe na mkombozi.

¹³⁵ Ijapokuwa alijeruhiwa, akavunjwa, akapigwa, akararuliwa, bali alijua njia ya kurudi nyumbani. Kwa hivyo kutoka kwenye msalaba wa kalvari walikomchubulia, wakamponda-ponda, wakamrarua-rarua kama kundi la mbwa-mwitu juu yake, yeye aliruka kutoka kalvari na kutua kwenye milango ya Mbinguni, akisema, “Imekwisha! Imekwisha! Wao wako huru! Ugonjwa unaweza kuponywa sasa! Wenye dhambi wanaweza kuokolewa! Walio kifungoni wanaweza kuwekwa huru!”

¹³⁶ Ingawa yeye alichubuliwa na kujeruhiwa, vile vita vikuu pale ambapo hata kila kitu kilikuwa dhidi yake...Hata yule mwanashairi alilia kwa sauti kuu:

Huku miamba ikipasuka na mbingu zikitiwa
giza,
Mwokozi wangu aliinamisha kichwa Chake
akafa;
Bali pazia iliyofunguka ilifunua njia ya
Kuelekea furaha za mbinguni na siku isiyo na
mwisho.

¹³⁷ Nimekuwa na ugojwa wa neva maishani mwangu mwote. Nilipokuwa mvulana mdogo kuna kitu kilichonipata, ambacho kila baada ya miaka saba hutendeka kwangu. Ndugu Jack anakumbuka nilipoanza kwanza, niliondoka uwanjani kwa muda wa mwaka mmoja; kitu fulani kilitendeka.

¹³⁸ Nakumbuka siku ambapo Juanita Hemphill...nafikiri jina lake ni Juanita Kelly sasa, yeye aliolewa na Ndugu Kelly baada ya kifo cha mumewe. Anna Jeanne, nina picha zao na kadhalika, walikuwa...Na...Na hao wasichana wawili na Dada Moore walikuwa wakiimba wao wa—watatu. Waliuimba huo wimbo ambao sisahau kamwe: *Kutazama Ng'ambo ya Machuweo*. Ndugu Jack, wakumbuka, nadhani, tulipokuwa tukija kutoka Florida. Wasichana wazuri vipi.

¹³⁹ Nami nakumbuka asubuhi hiyo kundi ndogo la Kipentekoste kutoka hapa upande wa kaskazini wa nchi hii, kule Michigan mahali fulani, hao wasichana walisimama kule nje wakati Ndugu Hooper...nalimwona usiku uliopita, mimi...huenda asiwe hapa sasa, Ndugu Ed Hooper. Uko hapa, Ndugu Ed? Sidhani yeye...Aliketi hapa usiku uliopita. Hamna...Wengi wenu mnamjua. Mimi naye, na Ndugu Hooley, tulikuwa tukiondoka. Na wasichana hao wakisimama pale pembeni wakiuimba huo, wakatupa, kila mmoja, ua la waridi manjano ambayo walitoa kwenye nywele zao. (Hapo ndipo yule mwenda wazimu aliponywa kule chini, mambo makuu yalikwisha kutendeka.)

¹⁴⁰ Nilipokuwa nikija barabarani huku nikiwa mwenye furaha nilivyoweza kuwa, mara kikanipata; mwaka mmoja baadaye kabla sijarudi uwanjani tena, nusura kiniue.

¹⁴¹ Tangu nilipokuwa mvulana mdogo, kila mara nilisema sikujua ono lilikuwa nini. Mvulana mdogo, kila mara nilisema, "La—laiti ningalishikwa na huo usingizi mzito, na kumwona huyo, ningepata afya." Wakati huo...Kila mara nilitaka kwenda kwa Mayo kuona shida hiyo ilikuwa nini. Madaktari huko...

¹⁴² Tumbo langu huniuma sana; lo jamani! Ndugu Jack amenisaidia kuzunguka nyumba. Mimi huzunguka nyumba; na maji yaliyo kama moto matelezi yakibubujika kinywani mwangu. Na kuenda mimbarani, na kuwaombea watu waliokuwa wagojwa maradufu, nao wanaponywa. Wao wameiweka mikono yangu juu ya mtu aliyekuwa na kansa usoni

mwake, na hiyo kansa ikaondoka usoni mwake, akisimama pale; nami nilikuwa mgonjwa sana singaliweza hata kusimama.

143 Nanyi hamjui jinsi nimeteseka; uchovu wa akili. Umekuja kila baada ya miaka saba, maishani mwangu mwote. Hapo ndipo nilipo sasa, saba nane.

144 Kwa hivyo nili—nilikuwa nimehangaishwa sana; nikalia, nikataka radhi, nikasihi sana.

145 Nami nakumbuka hatimaye nilipofikiria nilikuwa na fedha za kutosha kwenda kwa Mayo kufanyiwa uchunguzi; wao walisema, “Hao watapata shida yako ni nini.” Mimi na mke wangu, na Becky nyuma kule. . . Sara alikuwa kitoto, kichanga sana. Nilikuwa tu nimeingia katika huduma yangu ya uponyaji. Nasi tukaelekea kwa Mayo.

146 Nikapitia kliniki. Na ule usiku uliotangulia . . . ningefanyiwa uchunguzi wa mwisho asubuhi iliyofuata, niliamka tu na nilikuwa nimeketi pale kitandani nikitazama huku na huko. Nami nikatazama mbele yangu, na palikuwepo mvulana mdogo, alifanana nami sana, yapata umri wa miaka saba; basi nikamtazama, na ilikuwa mimi. Naye alikuwa amesimama karibu na mti wa mtoni. Na juu ya mti huo . . .

147 Ye yote wenu wawindaji wa kuchakulo anajua unaweza ukaparua kijiti kwenye mti kama huo hivyo, nako kutamstusha kuchakulo na kumfanya atoka humo kama yumo katika hilo shimo.

148 Nami nilikuwa nikitazama mle ambamo kuchakulo huyo alikuwemo, nami nikawaza, “Huyo ni kuchakulo wa aina gani?” Nami nikakiparua. Na nilipofanya hivyo, nikatazama basi na ilikuwa mimi yapata umri wa miaka thelathini na minane, huyo mvulana mdogo alikuwa amekwisha kuondoka. Kwa hivyo nikaparua tawi hilo, na kutoka kwa gogo hilo lenye shimo, mti, akaja kuchakulo mdogo yapata urefu huu, mweusi kidogo, karibu mweusi, na ilionekana kama mawimbi madogo yalikuwa yakitoka kwake; mwenye macho madogo yenye kung’aa sana, kitu kiovu sana nilichopata kuona, alionekana zaidi kama cheche kuliko kuchakulo.

149 Naye akanitazama moja kwa moja. Nami nikafungua kiywa changu kusema, “Vema. . .” Na nilipofanya hivyo, yeye. . . kabla hujafumba na kufumbua jicho lako, akaruka hata kinywani mwangu, akaingia tumboni mwangu, na kuninyambua. Na nilipotoka kwenye hilo ono, huku mikono yangu imeinuliwa juu, nikitazama, nikalia kwa sauti kuu, Ee, Mungu unirehemu! Ananiua”!

150 Nami nikasikia sauti kule ndani kabisa chumbani, ikisema, “Kumbuka, ina urefu wa inchi sita tu.”

151 Wangapi wamekwisha kusikia hadithi hiyo? Nimewahadithia nyingi, watu walio karibu na maskani.

152 Vema, ikaendelea na kuendelea, nikiteseka vivyo hivyo.

153 Mayo Brothers, siku iliyofuata, wakanifanyia uchunguzi. Kasema “Babako alikuwa Mu-Irish, alikunywa pombe. Mamako akiwa nusu muhindi, hiyo inakufanya karibu mtu aliyechanganyika damu. Kwa hivyo utakuwa . . . wewe ni—wewe ni mtu mwenye fadhaa sana hata haitakuacha kamwe.” Kasema, “La, sivyo, wewe una afya nzuri. Bali hicho, hicho ni kitu kilicho katika nafsi ambacho mwanadamu hawezi kuzuia.” Kasema, “Uta . . .” Kasema, “Mtu anapokufa, hiyo haiwezi kufanyiwa uchunguzi wa maiti, maana nafsi imekwisha kuondoka.” Yeye akasema, “Vema, haitakuacha kamwe.”

154 Na mtu huyo akasema, daktari wangu mzee, kasema, “Baba yangu alikuwa nayo, akafa akiwa na miaka themanini na mitano, miaka tisini,” kitu kama hicho, akasema. Naye akasema, “Mwezi mmoja au miwili kabla hajafa, nalimchunguza; alikuwa nayo maishani mwake mwote, angevipata hivyo” kasema, “vipindi vya fadhaa.”

155 “Watu wengine,” akasema, “wanapoipata, huwa na hasira ya haraka,” kasema, “hao ndio namna ya watu wanaoweza kukuua.” Akasema, “Aina ile nyingine, kama wanawake wanapoingia ugumba, wao hulia. Wewe una aina ambayo hujisikia mchofu.” Kasema watu wa kale walikuwa wanaiita, hali ya kuudhika, haingaliwaacha.” Hiyo inapokushika, tumbo lako linakuuma; unahangaika tu.”

156 Nikasema, “Lakini, bwana, sifanyi cho chote.” Nikasema, “Mimi huwa na furaha.”

157 Kasema, “Naam. Hiyo ni vikorokoro tu vya binadamu.” Kasema, “Utakuwa nayo daima.” Lo, ni jambo la kuvunja moyo jinsi gani!

158 Bali hayo maneno, ukiyawazia, “Kumbuka, ana urefu wa futi sita tu,” hayo sijayasahau, kama mke wangu mpenzi kule anavyoweza kuwaambieni. Mwaka baada ya mwaka, nimewaza hayo.

159 Ndiposa, nilipokuwa nikienda ng’ambo wakati huu wa mwisho nilikuwa . . . mbeleni. Vema, nilikuwa nimerudi nyumbani, nami nilikuwa katika safari ya kuwinda kuchakulo. Nikaruka kutoka katika motokaa pamoja na Ndugu Banks Wood, ambaye anasikiza usiku wa leo, na nikaanza kupanda kile kilima haraka, na ilionekana kwamba moyo wangu ungenitoka.

160 Nikamuuliza Dk. Sam Adair, nikasema, “Nini inasababisha havo?

161 Akasema, “Utakapoipata tena, nenda kafanyiwe uchunguzi wa moyo.”

162 Kasema, “Vema.”

163 Basi ikatendeka tena mwa—mwaka uliofuata, nami nikaenda na kufanyiwa uchunguzi wa moyo. Akasema, “Moyo

wako hauna kasoro,” kasema, “wewe unafadhaa tu.” Ikaaza wakati huo.

¹⁶⁴ Vema, daktari mwingine akaniambia, rafiki wangu sana, kasema, “Hiyo ni moyo wako, kijana,” kasema “unapaswa kujihadhari.” Huo ndio mwaka nilipompigia Ndugu Moore simu na akampata mtu kuhubiri badala yangu, nilipoenda kuwinda wale kondoo dume pamoja na Ndugu Fred. Nikapanda milimani kama tu nilivyofanya nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, maili baada ya maili, nikikimbia; haikunisumbua hata kidogo. Mwaona?

¹⁶⁵ Nami nikarudi na kumwambia Sam. Akasema, “Vema, kuna kasoro fulani, yakupasa kujihadhari.”

¹⁶⁶ Nikaona ono la daktari mzee aliyesimama na kile. . . daktari mtindo wa kikale akiwa na kile kisikizio cha vipigo vya moyo wako, mkononi mwake. Akasema. . . Alikuwa amesimama mbele yangu siku moja, akasema, “Usiache wakuambie ‘huo ni moyo wako, hiyo ni tumbo lako.’”

¹⁶⁷ Basi, ni—nikawaza, “Vema, nitaamini tu hilo neno, maana ilikuwa ono. Lililokuja.”

¹⁶⁸ Nikaanza safari ya Afrika, na kudungwa sindano, na ilinipasa kudungwa sindano kadha kabla sijaenda Afrika, hiyo ndiyo sheria. Basi, nilipokuwa nikidungwa sindano hizo, yeye akasema, “Naam, sioni kasoro yo yote kwako.” Kasema, wekundu wa damu yako, damu yako ni tisini na sita, ni tisini na sita.” Kasema, “Ungalikuwa na umri wa miaka kumi na sita, haingalikuwa bora zaidi, haingekuwa bora zaidi.” Naye akasema, “Moyo wa kutosha kukufikisha miaka mia moja. Mapafu, kila kitu,” kasema, “huna shida; hamna sukari, hamna kitu.”

¹⁶⁹ Nikasema, “Asante.” Kwa hivyo nikafanyiwa uchunguzi wa mwili na—na kupeleka ha—hati yangu ya daktari kwa halmashauri.

¹⁷⁰ Basi, akasema, “Unajua cho chote kuihusu?”

¹⁷¹ Nikasema, “Sijui kitu ila mwasho usiokwisha tumboni wakati wote.”

¹⁷² Akasema, “Vema, nitakwambia.” Akasema. . .

¹⁷³ Nikasema, “Ah, nimekwisha kufanyiwa uchunguzi. Nimewaendea Mayo Brothers, na kila mahali.”

¹⁷⁴ Akasema, “Lakini ngoja kidogo.” Akasema, “Mara kwa mara kidonda tumboni huwa kidogo sana hata madawa ya kuchunguzia hayawezi kukionyesha; na wakati mwingine ni kikumbwa sana hakiwezi kuonekana, kwa maana X—ray ni kivuli tu. Na kijidonda, hauwezi kukiona, hakiwezi kushikika vizuri. Vijidonda vingi vinaweza kufanya hivyo.” Akasema, “Namjua daktari mzee humu ambaye amevumbua chombo fulani, wanacho sasa; wanaweza kukufanya ulale kwa dawa

fulani kidogo ya magadi, waweke mrija kooni mwako, nao basi hata tumboni mwako waone kuna kasoro gani.” Kasema, “Yeye. . .” Akasema, “Ni moja wenu, yeye ni Mkristo.” Kasema Mbona usiende ukamwone.

¹⁷⁵ Nikachukua jina lake: Dk. Van Ravensworth. Kwa hivyo niliporudi, nikaenda kumwona huyo daktari mzee. Lo, ni daktari mzuri mzee kutoka Dutch East Indies, wa ukoo mkubwa wa kimishenari. Naye alikuwa amesikia habari zangu na kusoma kitabu changu, na lo, akanisalimia kwa mkono, akasema, “Ndugu Branham, ningefurahia kukufanyia hayo.” Akasema, “Hebu nikwambie utakayofanya; juma lijalo njoo huku hospitalini,” naye kasema, “na unipigie simu kabla hujaenda.” Naye kasema, “Ndipo nikifanya hivyo,” kasema, “inakufaya ulale kwa dakika tano.”

¹⁷⁶ Msichana wangu mdogo alikuwa tu amedugwa hiyo kusudi ang’olewe jino, na msichana mdogo wa Ndugu Norman. “Kulala kwa dakika tano,” nikawaza, “hiyo haitanidhuru.” Kwa hivyo, nikadhani nitaridhika basi, kuijaribu.”

¹⁷⁷ Ndipo asubuhi iliyofuata, niliamka kitandani na kutazama huku na huko, nikatazama kwenye hicho kitanda cha watu wawili, mke wangu mle, hakuwa ameamka bado. Nami nilikuwa nikitazama dirishani kuelekea milima mirefu ya Catalina ninakoishi, nami nikatazama kule ambako Malaika wa Bwana aliweka ule Upanga mkononi mwangu, ambako wale malaika saba mnaowaona kwenye ile picha walitokea, na mambo makuu yakatendeka.

¹⁷⁸ Nami nikatazama, na nilipokuwa nikitazama, nilikuwa nimesimama karibu na ule mti tena, pale pale yule kuchakulo alipokuwa. Nikatazama kule, nikawaza, “Lile ndilo lile tundu la huyo kuchukulo.” Nami nikawaza, “Nashangaa iwapo angali mle?” (katika ono). Nikaparuza upande mmoja wa ule mti, ndipo akatoka. Na kabla sijafumba na kufumbua jicho langu (yeye alikuwa kuchakulo wa kipekee sana niliyepata kumwona; naam, itakubidi ujue huduma yangu upate kujua mifano hii na kadhalika), yeye alinirukia bali hakunipata, akakikosa kinywa akagonga kifua changu na kuanguka.

¹⁷⁹ Na mara alipofanya hivyo, nikasikia kitu kikisema, “Nenda kwenye Milima ya Catalina.”

¹⁸⁰ Kwa hivyo nikageuka, nikasema, “Meda, u macho, Mpenzi?” Nami nikamwamsha.

¹⁸¹ Akasema, “Kuna nini?” Yapata saa kumi na moja usiku.

¹⁸² Nami nikasema, “Nilikuwa nikitazama kule nje, nami nikamwona yule kuchakulo tena, mpenzi.

¹⁸³ “Kuchakulo gani?”

¹⁸⁴ Nikasema, “Yule niliyemwona kule kwa Mayo.” Nikasema, Hakuupata mdomo wangu wakati huu, hakunipata, alianguka

kutoka kwa kifua changu.” Nikasema, “Bwana asifiwe! nimelitazamia, jamani, tangu nilipokuwa mvulana mdogo, nimekuwa na shauku sana kuona hilo likitendeka. Kama ningeona hilo likitendeka, si hata... Kabla sijajua ono ni nini, ningalionga hilo likitendeka, basi nikasema, ‘Nitakuwa mzima. Cho chote hilo lilichoniambia, hivyo ndivyo ningeikuwa.’ Na miaka arobaini nimetazamia hilo, na tayari limetendeka.”

¹⁸⁵ Hapo kabla, nilipokuwa kwa Mayo, wakati uo huo nilipokuwa kule waliponipa huo ujumbe, nami nikaona hilo ono...

¹⁸⁶ Maskini mama yangu amekwisha kwenda utukufuni sasa, mwanamke wa kipekee sana. Yeye alikuwa na ndoto tatu nne maishani mwake, nazo zote zilikuwa kweli kila mara. Yeye angeliniambia, na... Angalianza kuniambia, ningalimwambia... Ningesema, “Koma papo... Mama, nitakusimulia sehemu iliyobakia.” Mwaona?

¹⁸⁷ Maana kila mara unaponipa ndoto nikutafsiri, huniambii kila mara jinsi ilivyo hasa. Kisha ninapoiona yote tena, naona jinsi ulivyoona hasa, halafu yeye ananiambia ilivyo. Waona? Si lazima unieleze hiyo ndoto, Yeye Mwenyewe hunionyesha ilivyo. Waona? Ndiposa nikiiiona, nasema, “Vema, wewe hukuniambia *hili* na hukuniambia *lile*.” Waona? Kwa hivyo basi Mungu anayeweza kutafsiri ndoto, anaweza kuonyesha ndoto; Yeye anaweza kuionyesha moja, anaweza kuitafsiri. Na kwa hivyo basi...

¹⁸⁸ Vema, hapakuwepo jambo kama hilo katika Biblia, kasema, “Kama mnaweza...”? Na—na... Imenijia sasa hivi. Danieli, siyoy? La Yusufu—Yusufu. Vema iko mahali fulani katika Biblia. Nilikumbuka hiyo tu, kasema, “Kama mkinionyesha... kama mkiweza kuniambia jinsi... Oh, ni Mfalme Nebkadreza, hiyo ni kweli. Kasema, kama mnaweza... kama hamuwezi...”

¹⁸⁹ Wale wachawi wakasema, “Tusimulie sisi ile ndoto.”

¹⁹⁰ Yeye akasema, “Imeniondoka.” Hiyo ni kweli, hiyo, nakumbuka hiyo; nimeikumbuka sasa hivi.

¹⁹¹ Sasa tazama. Na mama, akasema, “Billy,” niliporudi, akasema, “njoo hapa, mwanangu, ukaketi chini.” Akasema, “Niliota ndoto ya ajabu. Naliota ya kwamba nilikuona wewe u-umelala ukiwa mgojwa, karibu kufa, tumbo lako kama kawaida.” Amenipikia vyakula vingapi! Naye akasema, “Ulikuwa ukijenga nyumba kilimani.” Naye akasema, “Naliwaona hua sita weupe wakishuka kutoka mbinguni, wakinong’oneza, katika herufu “S” nao wametua kifuani mwako. Nawe ulikuwa ukitazama, na yule aliyeongoza alikuwa akijaribu kukwambia jambo fulani. Kasema, walikuwa hua weupe waliong’aa sana. Wakaviinua vichwa vyao vidogo na kuviegemeza kwenye shavu lako, wakisema, “kuu, kuu, kuu.”

Akasema, "Singefahamu." Kasema "Waliendelea kusema, "kuu, kuu.

¹⁹² Nikasema, "Lo naiona, Bwana asifiwe!" Na kasema, "Wao wakafanya herufi "S" tena na kurudi juu mbinguni wakisema kuu, kuu, kuu,' wakirudi nyumbani."

¹⁹³ Vema, yule mnyama mdogo niliyemwona alikuwa mwenye urefu wa inchi sita. Huo mlolongo wa hua ambao Mama aliuona ulikuwa wa hua sita, sita si kamilifu. Nalijua ya kwamba siku moja nitamwona huyo wa saba. Hiyo ilikuwa mwanadamu, akiona maumivu; basi yakaendelea na kuendelea.

¹⁹⁴ Asubuhi hiyo, nikaamka baada ya kuona ono hili; nikamtii Bwana. Nikampeleka mtoto wangu, Yusufu, shuleni (anisikiza sasa, kule Tucson). Nikampeleka shuleni, na nikamwambia Meda sijui ningerudi lini.

¹⁹⁵ Nami nikaondoka kwenda Catalina, kule juu vilimani, na-nikaenda mahali ambapo Malaika wa Bwana alipoweka ule Upanga mkononi mwangu. Asubuhi na mapema; nami nikaanza kupanda huo mlima.

¹⁹⁶ Vema, badala ya kwenda kwenye vilele upande huu (ambako mna nyoka wengi, nge, mwajua Arizona ilivyo), nikageuka kulia; kitu kikasema, "Geuka kulia." Nikaenda kule juu kabisa vileleni; nikazunguka, nami nilikuwa nikizunguka hiyo miamba mikubwa mno, mikubwa mara nyingi sana kuliko maskani haya, iliyo kule juu sana ambapo ni shida kwa mtu ye kufika huko.

¹⁹⁷ Na yapata saa tano, nilikuwa nikiingia kwenye pango ndogo ambako...mahali padogo palipoingia hivi kwenye mkondo mdogo wa kulungu. Nami nilikuwa nimevua shati langu, kofia yangu mkononi mwangu, kwa sababu nilikuwa nimelowa jasho. Na kwa hivyo nikaingia, mle, na nilipokuwa nikiingia kwenye hilo pango ndogo, nikasikia uwepo wa Bwana. Kwa ghafla nikatoa kofia Yangu na kuangalia huku na huko. Nikawaza, "Yeye yuko hapa mahali fulani. Najua yeye yuko hapa." Nikawaza, "Ni nini?" Nikapiga hatua zingine chache. Nikasema, wewe uko hapa mahali fulani."

¹⁹⁸ Nami nikatazama hapo njiani, na yule kuchakulo mdogo alikuwa amelala pale; alikuwa amerukia kitu fulani akakikosa, na akagonga kijiti cha mpungate (hicho ni mpungate urukao). Kilijishindilia kichwani mwake, kifiani, tumboni, naye kafa. Huyo kuchakulo mdogo mwenye sura ya kuchukiza, alikosa mdomo wangu na kugonga hicho kijiti. Na Sauti ya Bwana ikasema, "Adui wako amekufa." Nilisimama pale, nikatetemeka. Nami nikainua mguu wangu na kum- . . .

¹⁹⁹ Kwa kawaida, kunguru angemla. Nalimuua nyoka, siku chache baadaye, alilala hapo njiani kwa yapata nusu saa. Kila wakati kuna tai na kunguru wanaoruka wakipita pale, nao watamchukua sasa hivi. Nalimuua nyoka wa marijani, huyo

ndiye nyoka hatari sana tuliye naye; alikuwa amelala karibu sana nami; siku chache baadaye. Nikaanza kurudi kumchukua nikamwonyeshane, kunguru walikuwa tayari wamemchukua, ndege waliokuwa wakipita pale.

²⁰⁰ Na huyo alikuwa amelala pale tangu nilipoona hilo ono, siku mbili hapo kabla; naamini ilikuwa Jumamosi, nami nilienda kule Jumatatu. Kwa hivyo alikuwa pale, amelala pale hali maiti. Nikamponda—ponda kwa mguu wangu.

²⁰¹ Nikarudi kule nikaketi tena; nikaketi na kulia kidogo, na kuomba; nikiutazama Tucson kule chini, maili kadhaa chini yangu.

²⁰² Nikageuka na kurudi, alikuwa yupo pale bado. Nilipoingia kwenye lile pango roho wa Mungu akanijia tena.

²⁰³ Nikazunguka, nikashuka mlimani. Nikaingia na kumwambia mke wangu, nikasema, “Mpenzi, sijui vipi, bali nitapona.”

²⁰⁴ Dk. Ravensworth, aliponifanyia uchunguzi, alisema, “Haiwezekani kabisa kwako kupata afya.” akanidunga ile sindano ya dawa yenye magadi ambayo ingalinichukua muda wa dakika tano, nami nikalala masaa kumi. Kwa hivyo kitu hicho, hata asprini hunibwaga chini. Kwa hivyo wao... Akanidunga sindano, akatia huo mrija kooni mwangu. Nilipopata jirudia, yeye akaniambia asubuhi iliyofuata, akasema, “Kasisi, nachukia kukwambia hili, bali” kasema “kuta za tumbo lako ni ngumu sana, zimekauka.” (Sikuziona; alitumia jina la gastritis, nami nilienda na kuliangalia kwenye kamusi na ilisema, “kitu ambacho kimenyauka kabisa”). Naye kasema, “Hauwezi ukapona.” Akasema, “Utakuwa nao daima.” Nami ningalikuwa mtu aliyeshushwa moyo kama haikuwa kwa ajili ya hilo ono la Bwana.

²⁰⁵ Na siku iliyofuata Kitu fulani kikasema, “Rudi kule mlimani.”

²⁰⁶ Na siku hiyo, badala ya kwenda njia moja, niliongozwa kupitia njia nyingine. Nami nilikuwa nimesimama pale; na nilipotazama, hapo mbele yangu, alikuwa yule hua mdogo mweupe, akinitazama. Nikapangusa macho yangu, nikasema, “Bila shaka, ni ono; bila shaka, ni ono.” Nikatazama, na kusema, mdogo, unatoka wapi?” Mzuri sana na mweupe, huenda alikuwa njiwa; cho chote alichokuwa, kule mbali katika hilo jangwa.

²⁰⁷ Mungu Mwenyezi, aliyemfufua Yesu Kristo katika wafu, Yeye ambaye mimi ni mtumishi Wake, na Neno Lake liko hapa limefunguliwa mbele yangu, anajua ya kwamba nasema kweli na sisemi uongo.

²⁰⁸ Hapo alitua huyo hua, akitua pale akinitazama. Nikazunguka pale, nikawaza, “Bila shaka, ni ono.” Nikageuza kichwa changu, nikatazama kule nyuma, naye alitua pale,

hizo mbawa ndogo, zilikuwa nyeupe kama theluji iwezavyo kuwa; miguu yake midogo, na ya kimanjano; na mdomo wake mdogo wa kimajano; ametua pale huku ananitazama. Yeye alikuwa akiangalia moja kwa moja magharibi. Nikamzunguka hivi, singalimguza kwa cho chote. Nikafuata huo mkondo; nikatazama nyuma, alikuwa pale bado anitazama.

²⁰⁹ Ndugu, kama mwana wa Ibrahimu, siangalii yale daktari aliyoniambia, nitapata afya, kwa vyo vyote!

²¹⁰ Siku ya tatu nikarudi, nilikuwa nikikwea juu sana. Na wengi wenu wanajua lile ono kuhusu chifu wa Kihindi akipanda farasi kwenye ule ukuta mdogo akielekea magharibi. Kitu fulani kikanivutia kwenye mwamba mkubwa, yapata wakati wa adhuhuri, kasema, “Weka mikono yako juu ya huo ukaombe.” Mungu aliye Mbinguni ajua hili ni kweli.

²¹¹ Nikaweka mikono yangu juu ya huo mwamba na kuinua macho yangu juu Mbinguni na kuanza kuomba, nami nikasikia Sauti ikitoka juu ya hiyo miamba pale, kasema, “Unauegemezea nini, moyo wako?” Nami nikainuka hivi, mabega uchi; uchi tangu kiunoni kwenda juu, joto. Nikatazama nyuma. Na ilikuwa imeandikwa kwa kito cheupe, kwenye jiwe, “Tai Mweupe,” kile lile ono lilisema kingeleta Ujumbe wa pili.

²¹² Nikajawa na furaha, nikakimbia nyumbani, nikachukua kamera na kurudi siku iliyofuata na kuipiga picha. Ilikuwa ingali pale, imeandikiwa katika mwamba: “Tai Mweupe.” (Hua akimwongoza tai).

²¹³ Kwa njia isiojulikana, na—najua. Nitawaambieni kabla haijatendeka. Huyu daktari ni daktari mzuri. . . daktari mzuri, shaka; na—nafikiri ni mtu mzuri. Bali na—najua ni—nitapata nafuu. Imetendeka! Imekwisha, nami nitapata afya!

²¹⁴ Nalikuwa nikiwaza wakati Ernie alipokuwa akiimba huo wimbo muda mfupi uliopita, *Juu ya Mbawa za Hua*. Sauti yake ikoje? Uanzishe kwa ajili yangu, Ernie.

...mbawa...hua mweupe kama theluji,
(imbeni pamoja nami)
Mungu alituma upendo Wake msafi na mtamu,
Ulikuwa ishara toka juu,
Juu ya mbawa za hua.

²¹⁵ Nimefahamishwa ya kwamba Ernie alijitungia aya mbili zake Nami nitawatungieni aya tatu:

Nuhu alichukuliwa
Juu ya gharika siki nyingi,
Alitafuta nchi kavu,

Kwa njia mbali mbali;
 Shida alizipata,
 Bali si kutoka juu,
 Maana Mungu kampa ishara Yake
 Juu ya mbawa za hua.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu alituma upendo Wake msafi na mtamu.
 Ulikuwa ishara toka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

Yesu, Mwokozi wetu
 Alikuwa duniani siku moja;
 Akazaliwa zizini,
 Katika hori la majani makavu;
 Ingawa hapa alikataliwa,
 Bali siku toka juu,
 Kwa maana Mungu alitupa ishara Yake
 Juu ya mbawa za hua.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji.
 Mungu alituma upendo Wake msafi na mtamu
 Lo, ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

Ingawa nimeteseka
 Katika njia nyingi,
 Nalililia uponyaji
 Usiku na mchana pia;
 Bali imani haikusahauliwa
 Na Baba aliye juu,
 Yeye akanipa ishara Yake
 Juu ya mbawa za hua.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu alituma upendo Wake msafi na mtamu
 Lo, ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu ilituma upendo Wake msafi na mtamu
 Ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

²¹⁶ Mungu mpendwa, nakushukuru kwa mambo haya, Baba. Ulimpa Nuhu ishara, uliupa ulimwengu ishara, nawe ulinipa ishara. Na siku iliyofuata, nilipoona huyo tai akiruka, Ee, kuna Ujumbe unaokuja sasa, nami naomba, Mungu, ya kwamba utamwacha Hua aongoze. Tujalie, Bwana. Imeniongoza kwa imani ambayo sikuwa nayo hapo awali. Najua, Mungu, najua itakuwa sawa, kwa hivyo nakushukuru kwa ajili yake, Baba.

²¹⁷ Na, usiku wa leo, tutumie Ujumbe Wako tena, Bwana, kwa mbawa za Hua wa Neno. Tujalie, Baba mpendwa wa mbinguni.

Na kila mtu anayepita jukwaani humu, usiku wa leo, na kule nje katika mikutano kote nchini, na Hua Wako mkuu wa imani aingie mioyoni mwao akawape imani, Bwana, kwa ajili ya uponyaji wao. Kumbuka ya kwamba Mungu hana upendeleo. Angeweza kuutuma huo ujumbe kwa Nuhu, angeutuma kwa Yohana Mbatizaji, angeutuma kwangu, anaweza kuutuma kwa wengine.

²¹⁸ Naomba ya kwamba huyo Hua ataruka aingie katika kila moyo sasa hivi, Bwana, akiwa na mdomo wake mdogo wa dhahabu, akawanong'onezee ya kwamba, "Kwa kupigwa kwake... Kwa majeraha yangu na kupigwa kwangu impeponywa." Mungu, tujalie yakwamba makosa yetu yatafutuliwa mbali, maovu yetu yatasamehewa, na ya kwamba magonjwa yetu yataponywa. Iko mikononi mwako, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Vichwa vyenu vikiinamishwa kwa dakika moja zaidi:

²¹⁹ Wangapi hapa wangetaka kusema, kama waweza na wataka kusema hili, "Ndugu Branham, nimekosea maishani mwangu mwote. Nimetaka kumtumikia Mungu, bali usiku wa leo mimi niko tayari kujitoa. Mwombe Mungu, ya kwamba huyo Hua ataruka aingie moyoni mwangu usiku wa leo. Naweza kumsikia akipigapiga mbawa Zake anapoingia"? Inueni mikono yenu, Hapa kwenye kusanyiko linalooneka: jamani, kote, jengoni.

²²⁰ Kote kwenye wasikizaji nchini, kote hata kwa akina Ndugu na Ndugu Coleman, kule kwa Ndugu Leo na wengineo, kule Tucson, hata kwa maskani ya Branham, kote katika Pwani ya Magharibi, inueni mikono yenu kila mahali: "Nataka Hua akaruke aingie moyoni mwangu usiku wa leo. Akaniletee upendo mtamu wa Mungu juu ya mbawa za Hua mweupe kama theluji, huyo Roho Mtakatifu. Mlete kwangu, usiku wa leo, Bwana, na ukamiminie moyoni mwangu imani ninayohitaji."

²²¹ Katika Jina la Yesu Kristo, naomba, Mungu, utusamehe dhambi zetu. Yule Hua aliyejeruhiwa ameurdisha Ujumbe, Ee, Mungu, "Imekwisha!" Tunaamini hayo. Hebu na utupe imani kuamini tukauamini huo tunaomba. Katika Jina la Yesu. Amina.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
Mungu alituma upendo Wake msafi na mtamu,
Ulikuwa ishara kutoka juu,
Juu ya mbawa za hua.

²²² Huyo hua alikuwa ametoka wapi? Sijui. Hangalikuwa mle jangwani hivyo. La, la! la, hangalikuweko kule. Na kwa nini alikuwa mweupe? Mungu wa mbinguni anajua alikuwa mweupe kama shati langu. Alitua pale.

Bali ilikuwa juu ya mbawa za hua mweupe
 kama theluji,
 Mungu alituma upendo wake msafi, na mtamu,
 Lo, ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua,
 Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu alituma upendo wake msafi, na mtamu,
 Lo, ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

²²³ Jamani, hamjisikii wanyenyekevu sana? Na tusalimiane kwa mikono sisi kwa sisi, tukauimbe:

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji
 Mungu alituma upendo Wake msafi na mtamu,
 Ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

²²⁴ Na tumwinulie yeye mikono, tukauimbe:

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu alituma upendo Wake msafi na mtamu,
 Ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

Nuhu alichakuliwa
 Juu ya gharika siku nyingi,
 Alitafuta nchi kavu,
 Kwa njia mbali mbali;
 Shida alizipata,
 Bali si kutoka juu,
 Mungu kampa ishara yake
 Juu ya mbawa za hua.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu alituma upendo Wake msafi na mtamu,
 Lo, ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

Yesu mwokozi wetu
 Alikuwa duniani siku moja;
 Akazaliwa zizini,
 Katika hori la majani makavu;
 Ingawa hapa alikataliwa,
 Bali siku kutoka juu,
 Mungu akatupa sisi ishara Yake
 Juu ya mbawa za hua.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu alituma upendo Wake safi na mtamu,
 Ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua,

²²⁵ Mbona mimi niliye mzee, nikateseka maishani mwangu mwote, mbona yeye akaniponya sasa? Naamini nitarudia njia hii

tena, sina budi kuleta Ujumbe! Nami namwambia Baba yangu, usiku wa leo, (kama Junior alipoona ka—katika ndoto usiku mwingine kuhusu mbawa za huyu Hua akiruka kwenye hizi dirisha hapa), Bwana, mtumishi wako yuaja akatumike. Amina, niko tayari!

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu,
Ishara kutoka juu,
Juu ya mbawa za hua.

226 Na tuaminini sasa ya kwamba Yeye yuaja juu ya kusanyiko.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji . . .
(tunasubiri, Bwana)
Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu
Ishara kutoka juu
Juu ya mbawa za hua.

227 Ninyi mlio na kandi za maombi, katika marefu haya hapa, mbele hapa; simameni, mkajongee mbele katika marefu haya hapa, upande huu.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu,
Ishara kutoka juu,
Juu ya mbawa za hua.

228 Wale walio na kandi za maombi katika mstari huu, nendeni upande wenu wa kushoto.

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
Mungu huituma upendo Wake msafi na
mtamu,
Ishara kutoka juu,
Juu ya mbawa za hua.

229 Wale . . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh].

Lo juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
Mungu alinitumia upendo Wake msafi, na
mtamu,
Ishara kutoka juu,
Juu ya mbawa za hua.

230 Je, huyo hua alitoka wapi mle juu katika jangwa? Ningesema hivi: Mungu aliona ya kwamba Ibrahim alihitaji kondoo dume kama ishara, Yeye ni *Yehova-yire*, “Bwana atajipatia Mwenyewe hiyo sadaka.” Kuwazia hilo! Mungu yule yule, kwa kutiwa pumzi kule kule, kwa watu wa tabaka ile ile, hua. Yeye yungali Mungu, Yohova-yire anaweza kujipatia cho anachohitaji.

231 Mbona wewe, wakati tu unapopitia mstari huu wa maombi, usimuulize Mungu akupatie juu ya mbawa za Hua? Huyu Hua, Roho wa Roho Mtakatifu, akupe imani moyoni mwako upate kuamini ya kwamba utaponywa.

²³² Ninajaribu kuwafanya wote wasimame, mwaona. Nauliza sasa. Ndugu Brown yuko kwake. Ndugu Jack... Unasemaje? [Mtu fulani anamzungumzia Ndugu Branham—Mh.] Vema, sawa. Sehemu *hii* hapa, itapitia upande *huu* kwanza, ambao wamefanya mstari. Sehemu hizi nyuma *humu* watawafuata. *Hawa* watafuatia upande huu. *Nanyi* mfuata hawa hapa, mkija moja kwa moja humu mkaombewe.

²³³ Naam, naamini huu hautakuwa mstari unaoenda haraka kamwe, tutachukua tu wakati mdogo ili tupate kumwombea kila mmoja, tuwezavyo.

²³⁴ Sasa, naliufupisha ujumbe wangu kidogo (nanyi nyote mlipapata hilo, mwaona) kusudi nipate kuwa na mstari huu wa maombi Huu ni mstari wa kumbukumbu ya heshima ya siku ambazo Ndugu Jack Moore, Ndugu Young Brown, wake zenu waliwaruhusu kwenda, nanyi mkaja na tukaingia California, na kote katika Arizona (Pamoja, kupitia jangwani) na kuombea wangonjwa.

²³⁵ Mwajuaje? Mna watu wanaoishi leo waliokuwa wanakufa wakati huo, na wangali hai kwa sababu ya juhudi hiyo. Ilifanyaje? Ikaleta uponyaji wa Kiungu katika kila kanisa lililomo nchini, sasa hata Wapresbeteria na kadhalika. Wao... Ilinyamazisha midomo yao, kwa sababu ilimhitaji Mungu kumtia mafuta mtu fulani apate kumua Goliathi, kuonyesha ya kwamba ingeweza kutendeka, ndipo wengine wao wakajipa moyo (hiyo ni kweli) na wakasonga mbele. Inaweza kufanywa tena, kwa maana Yeye yungali anatuma upendo Wake juu ya mbawa za Hua.

²³⁶ Wakristo, nawatakeni msikize. Ningelisimama hapa na kujaribu kuwanukuulia mambo ya kimbinguni ambayo nimeona yakitendeka hata katika miaka mitatu iliyopita, ningekuwa hapa wakati kama huu Jumamosi ijayo, nikiwasimulia. Hata sineni habari zake sana, kwa maana huonekana kama kwamba hayawezekani, bali nawaambieni yaliyo kweli. Ni kweli hasa. Tunaishi chini ya uongozi wa Yehova Mkuu aliye mwenye nguvu, yeye yule aliyekuwa na nabii katika Agano la Kale, pamoja na Kanisa katika Agano Jipya, Yeye yuko hapa leo akitoa Bibi-Arusi kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake. Aminini! Sivyo, enyi watu? Iwapo uliwahi kuliadini, liadini sasa. Hapo ndipo... Nawatakeni mfanye hivyo. Hatujui bado yatakayotendeka usiku huu. Hatujui bado yatakayotendeka. Tunangoja tu tukiwa na matarajio.

²³⁷ Tafadhalini, katika Jina la Bwana Yesu, nawaulizeni kama mtumishi Wake. Najua unaposhughulikia kusanyiko, mna kila kitu kimechanganyikana mle. Bali iwapo mnaniadini mimi kama mtumishi Wake, iwapo mna shaka hata kidogo (ama *dhambi* ni—ni “shaka, kutokuadini”), iwapo mna chembe moja yake mwako, mwombe Baba aiondolee mbali sasa hivi. Waona?

“Bwana . . .” Unapokuja na imani halisi . . . Sasa, mikono yangu haitamaanisha kitu isipokuwa Hiyo ikuguse kwanza; Basi inapokuja, itaiangazia, nawe utaponywa. Hiyo ni kweli, utajua utaponywa. Waona, utaiamini.

²³⁸ Sasa, nitaomba sasa kwa ajili ya kila mmoja wenu. Nami . . . Mnapofanya hivyo, mnawekeana mikono ninyi kwa ninyi pia, tupate . . . Nawe mwombe mtu uliyemwekea mikono, ndipo nitawapisheni mstarini. Weka mikono yako juu ya mtu fulani aliye pamoja nawe mstarini.

²³⁹ Mungu mpendwa, si—sijui njia nyingine yo yote ya kusema mambo haya, Bwana. Najua tu kusema ninayojua kuwa ni kweli, Nawe u shahidi wangu ya kwamba ninasema kweli. Imani yangu, Bwana, na uponyaji wangu siku za usoni, sijui lini, sijui vipi, silifahamu; bali naamini Hilo, Bwana, ya kwamba nalipokea ishara kutoka juu. Huyu hua wa saba hatimaye alifika humu, ile inchi ya saba imetimizwa hivi karibuni kwa huyo mnyama. Imekwisha!

²⁴⁰ Mungu, nataka kuwatumikia watu Wako. Kwa hivyo naomba, Mungu, ya kwamba utatutia mafuta usiku huu ili kwamba ye yote tutakayemwekea mikono yetu, na waponywe; si kwa sababu ni sisi, bali kwa sababu ni kufuata amri Zako. ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Bwana, nisaidie kuamini, na uisaidie mioyo yao ipate kuwa tuta ya imani. Na iwe, pamoja, kwa utukufu wa Mungu, kila mtu mgojwa na anayeteseka katika jengo hili (ama mijengo kote nchini) ambaye anatii amri hizi sasa, atapata afya. Katika Jina la Yesu naomba hayo. Amina.

²⁴¹ Iweni na imani; nyote ombeni pamoja nasi. Naam, huu si wa mstari wa upambanuzi.

²⁴² [Mahali patupu kwenye utepe—Mh.] Huzuni, uoga, najua kile huyu . . . Maskini mwanamke huyu, alisema hajapata amani maishani, jambo lile lile ambalo . . . ? . . . hawezi kulala anashikwa na fadhha, ana wasiwasi.

²⁴³ Mungu mpendwa, nishuhudie, Bwana, ya kwamba nimesema kweli. Jinsi ninavyomwonea huruma maskini mama huyu! Naomba Mungu, ya kwamba utamtumia, usiku huu, huo mwali wa imani utokao juu ambao unajua ya kwamba Wewe una wajibu kwa Neno Lako, na utatimiza kila Neno. Mungu wa Mbinguni na aondoe uoga huu kutoka kwa dada yangu. Nami nakutii Wewe kwa kuweka mikono yangu juu yake na kuuhukumu. Katika Jina la Yesu Kristo, na umtoke. Amina.

²⁴⁴ Sasa, tazama dada, wewe niamini sasa, ukiweza kuanza kutoka papa hapa, karibu na msalaba. Tangu usiku huu, wewe kataa ya kwamba unao. Waona, endelea kusema, “Sina huo tena.” Kisha utakuacha.

²⁴⁵ Dada Palmer, dada yetu, Dada Palmer; bwana yake ni rafiki msiri wangu, mhudumu kutoka Georgia ama Alabama,

Georgia—Georgia. Alikuwa yuaja maskanini... Wao huja kwa motokaa, ninapohubiri kule maskanini, maili elfu moja mia tano kusikiza ibada moja. Ndugu Palmer alishindwa kuendesha motokaa yake, ama yule kijana, mmoja wao, walipokuwa wakikata kona, nao wakapata ajali. Huyu angali anaumia kwake. Na tuombe:

²⁴⁶ Mungu mpendwa, mponye huyu mtumishi Wako, maskini mke wake, mwaminifu, wa kweli, mtumishi mdogo katika Kristo, naomba, Mungu ninapomwekelea mikono yangu pamoja na Ndugu Jack Moore hapa, ya kwamba utamponya na kumpa afya. Katika Jina la Yesu. Amina.

²⁴⁷ Katika mguu wa kuume, nawe unasimama mahali pake? Mtoto wake ni kiwete, naye anaumwa na tumbo lake na mgongo pia. Na tuombe:

²⁴⁸ Mungu mpendwa, na huyo Hua mweupe kama theluji aingie kwenye kilindi cha moyo wake sasa, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Naomba hii iwe hivyo kwa ndugu yetu na mwanawe mdogo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁴⁹ Kuumwa sana na kichwa pamoja na maumivu, na maradhi ya mguu ambayo humsumbua anapofanya kazi.

²⁵⁰ Mungu mpendwa, jalia baraka Zako za uponyaji huyu kijana mwanamume sisi kama watumishi wa Mungu tunapoweka mikono yetu juu yake. Katika Jina la Yesu Kristo Amina.

²⁵¹ Yeye yuna shida ya wanawake, kike, na pia anataka ubatizo wa Roho Mtakatifu.

²⁵² Mungu mpendwa, ninaomba dua hii ya imani kwa ajili ya maskini bibi huyu, na shida hiyo ya kike iondoke, hebu ubatizo wa Roho Mtakatifu uje juu ya mbawa za Hau, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. (Mungu akubariki, dada)

²⁵³ Kivimbe juu ya jicho lake na kwa ajili ya mpenzi mwenziwe.

²⁵⁴ Mungu mpendwa, wewe unajua mioyo ya binadamu. Nakuomba Ewe Baba, katika Jina la Yesu, ya kwamba utatujalia haja hii ambayo huyu ndugu ameomba, na kutii kwetu Neno Lako kwa kumwekelea mikono. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina. (Mungu akubariki, ndugu)

²⁵⁵ Yeye yuna kivimbe upande wake wa kushoto, na pia sauti yake ni baya.

²⁵⁶ Yesu mpendwa, naomba ya kwamba utamponya huyu dada; tunapomwekelea mikono katika Jina la Yesu Kristo, ili apate kupona. Amina. (Mungu akubariki, dada yangu)

²⁵⁷ Masikini dadangu, naona shida yako, kiungo kilichovimba. Figo, kibofu, na kifundo cha mguu kilichotenguka.

258 Ee, Baba, Mungu, mponye mwanamke huyu mpendwa, Bwana, naomba, ninapomwekelea mikono katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

259 Mungu akubariki, dada; hivyo ndivyo ipasavyo, itatendeka.

260 Mnasikia hayo, sivyo, kwenye maikrofoni? Ye yote yule aliye...fundi wa mitambo, kama utaiongeza sauti kidogo, kusanyiko wapate kusikia ushuhuda wao...ama wanavyosema wanapopitia hapa. Waombeeni mnapousikia; ninapoanza kuomba, ombeni pamoja nami.

261 Mungu mpendwa, namwombea huyu dada yetu, ya kwamba utamponya, Mungu mpendwa. Tunafanya haya kwa maana ni amri Yako. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

262 Mungu mpendwa, wewe umesikia ushuhuda huo, umesikia yale adui amemtendea. Tunajaribu kulichukua Jina la Yesu tukamshinde huyu adui, tayari ameshindwa kwa maana Hua aliyechubuliwa, akavuliwa nguo, alianguka sakafuni mwa nyumba ya Mungu akiwa na Ujumbe, "Imekwisha!" Tujalie, hebu yeye aamini hivyo, Baba, katika Jina la Yesu.

263 Mungu mpendwa, naomba ya kwamba Wewe utamponya huyu dada yetu. Na hua wa Mungu amshuhudie usiku huu ya kwamba Yeye alitenda hayo kwa ajili yake, apate kupata afya. Katika Jina la Yesu. Amina.

264 Mungu mpendwa, naweka mikono yangu juu ya ndugu yangu anayesimama hapa. Yeye alikuwa na imani kutosha kuja umbali huu, Bwana, hebu sasa apokee uponyaji wake na aende akaketi ali mzima katika Jina la Yesu.

265 Mungu mpendwa, namwobeia ndugu yetu, nikimwekelea mikono. Saidia, Mungu mpendwa, ya kwamba imani ya Mungu itashuka chini wakati huu; na awe kama Ibrahimu, aliyeita mambo yaliyoko, kama ha—hayakuweko, kwa maana Mungu alifanya ahadi. Katika jina la Yesu. Amina.

266 Mungu mpendwa, Wewe ndiwe unayeweza kufanya uamuzi wa kweli. Naomba, Mungu mpendwa, kwa maana huyu bibi mdogo aliomba hili, hebu na alipokee katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

267 Mungu mpendwa, naweka mikono yangu juu ya dada yetu katika kutii yale uliyosema tufanye. Hii inaturudisha nyuma miaka mingi, Bwana, tangu tulipofanya mstari wa maombi kama huu; tunajua yaliyotendeka wakati huo, tunajua Wewe ni Mungu yule yule leo kama watu wanaweza kuwa na imani ile ile leo. Naomba katika Jina la Yesu kwa uponyaji wa dada yetu. Amina.

268 Mungu, mpendwa, naiweka mikono yangu juu ya ndugu yangu hapa na kuomba apate kupona, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

269 Baba, namleta mbele Yako usiku wa leo huyu dada yetu, na kuweka mikono yangu juu yake kushuhudia ya kwamba

ninasimama kama shahidi wa nguvu Zako, nasimama kama shahidi wa maono Yako, Neno Lako, nami ni shahidi ya kwamba Wewe ni Mungu. Nami naweka mikono yangu juu yake katika kutii Neno la Mungu wangu, na naomba apate kupona. Amina.

²⁷⁰ Mungu mpendwa, naweka mikono yangu juu ya ndugu yangu vivyo hivyo, kama shahidi wa nguvu Zako naomba apate kupona katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁷¹ [Mahali patupu kwenye ukanda—Mh.] “Nini?”

²⁷² Yeye alisema, “Mponyaji.” Akasema ya kwamba “Mtu fulani kutoka mahali fulani, huko Arkansasa, alikwisha kuponywa asubuhi hivyo, kipofu mtengenezaji wa viatu.” (mnajua hadithi hiyo, ilikuwa redioni).

²⁷³ Nami nikasema...Nikawaza...Nalitenda kama mnafiki. Nikasema, “Je, hauamini hiyo ni kweli?”

²⁷⁴ Yeye akasema, “Naam, bwana, naamini.”

²⁷⁵ Nami nikasema, “Je, unaamini katika siku hii wakati Mungu angefanya kitu kama hicho wakati...”

²⁷⁶ Yeye akasema, “Bwana, nalisikiza kipindi cha dini.” Akasema, “Mimi ni Mkristo.” Akasema, “Nalisikiza vipindi hivyo, nikamsikia huyo mtu kule aliyeponywa asubuhi hii, huyo kipofu mtengenezaji viatu. Wao walimfukuza kanisani, alikuwa akipiga kelele sana, kutoka kanisa moja kuingia lingine. Huku akiweka kofia yake kwenye bakora, na kuizungusha huku na huko, akikimbia juu chini kanisani. Alikuwa kila mahali mjini akipaza sauti na kusema, “Nimeponywa! Nimeponywa Kipofu mtengenezaji viatu.”

²⁷⁷ Nikasema, “Unaami hilo?”

²⁷⁸ Naye akasimama pale kidogo, kulikuwa na manyunyuyu ya mvua, akasema, “Bwana, ukinipeleka mahali aliko, ndipo nitamwona Baba yangu.” Ndipo nikajisikia *hivi*.

²⁷⁹ Nikasema, “Huenda ikawa mimi ndiye unayemtafuta.”

²⁸⁰ Akasema...akanishika ghafla kwenye kunjo la koti langu kifuani, akasema, “Wewe ndiye huyo mponyaji?”

²⁸¹ Nikasema, “Sivyo, dada, bali mimi ni Ndugu Branham.”

²⁸² Yeye akasema, “Unirehemu!” Nikawaza juu ya maskini kipofu Fanny Crosby, “*Unapozuru wengine usinipite.*” Mwaona, alikwisha kuponya mmoja, Yeye angemponya huyo mwanamke.

²⁸³ Nikaweka mikono yangu juu ya macho yake, nikasema, “Yesu mpendwa, siku moja msalaba wa kale usio laini ulikuja ukifanya vishindo barabarani, mabega yakitoka damu, mwili huo mnyonge ambao ulianguka chini ya mzigo huo. Mtu mmoja mweusi jina lake Simoni, Mkirene, akaja na kuutwaa huo msalaba, akamsaidia kuubeba. Nina hakika unakumbuka hayo, Baba. Na mmoja wa watoto Wake anapepesuka hapa gizani, nina hakika Wewe unafahamu.”

284 Yeye akasema, “Mungu atukuzwe! Naweza kuona!” (a—haa)

285 Nikasema, “Waweza kuona?”

286 Akasema, “Naam, Bwana.”

287 Nikasema, “Hesabu hizi taa.” Naye akazihesabu. Nikasema, “Suti yangu ni ya rangi gani?”

288 Akasema, “Una suti ya kijivu, na tai ya kimajano.” Ndivyo ilivyokuwa, yeye angeona.

289 Lo, Mungu huheshimu unyenyekevu (a—haa):

*Na hili lenyewe ndilo litakalosababisha, na kutimiliza,
ule ushindi mkuu katika Upendo wa Kiungu.*

290 Mungu mpendwa, mrehemu na kumponya dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina

291 Mungu mpendwa, ninapouchukua huu mkono mnyonge, wenye kunyanzi, ni wewe tu unayejua yaliyopitia hapa. Naomba, Mungu mpendwa, ya kwamba mkono uu huu nilio nao usiku huu utakumbatia kama ile mikono minyonge ya Simeoni siku hiyo, “Bwana, wamruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani, kwa kuwa sasa nauona wokovu Wako.” Na uje juu yake, Bwana, wokovu Wako, na kuponya katika Jina la Yesu. Amina.

292 [Sehemu tupu kwenye ukanda—Mh.] Kuhusu “*Ile Hukumu*, Bw. Kutokuamini alimshtaki Yesu Kristo. Mnakumbuka *Ile Hukumu*?” Ambavyo wao... Wao walikuwa na—na hikimu na kila kitu, na ni nani aliyesimamia nani. Na walikuwa na—na wakili wa mashtaka, Shetani, ambaye angefanya mashtaka; jinsi hiyo hukumu ilivyoendeshwa.

293 Naye akasema, mmoja, Bw. Mashaka, akajitokeza, akasema, “Nalimsikia mhubiri akisema, “Paka walio wagojwa mafuta, Bibilia inasema hivyo. Mimi nilipakwa mafuta, sikupona. Huyu mwingine akasema, Weka mikono juu ya wagojwa, na watapata afya.” Yeye alikuwa akijaribu kushtaki.

294 Bali shahidi alipojitokeza, ilikuwa hivi, “Mungu aliwaambia akasema, ‘Mlikuwa...’” Yeye akasema, “Ni miezi sita tangu nilipowekelewa mikono, na Neno Lako husema Wekeni mikono juu ya wagonjwa nao watapata afya.’ Nami niliwekelewa mikono na mmoja wa watumishi Wako waliopakwa mafuta, sijapata afya bado. Kwa hivyo Wewe ni mdai wa uongo, kwa maana Neno Lako halimaanishi lisemavyo.”

295 Basi shahidi alipokuja, ukweli ulikuwa huu, ya kwamba “Neno Lake ni kweli. Yeye hakusema kamwe ni lini atakapotekeleza hilo, Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: wakiweka mikono yao juu ya wagojwa, wao watapata afya.” Mwaona? Mwaona, hivyo ndivyo Yeye alivyosema, “Watapata afya.” Kwa hivyo kama ni muujiza wa mwelekeo kama huu ambao umetendeka hivyo tu au ni kumtii tu Mungu, hiyo ni juu Yake katika mtu binafsi. Mwaona?

Bali kama mtu binafsi akiliamini, sijali itachukua muda gani. Yeye alimwambia Ibrahimu, “Utapata mtoto kwa Sara.” Huyu mtoto hakuja kwa miaka ishirini na mitano. Yeye alimwambia Nuhu mvua itanyesha. Nuhu akawa na gharika...sa—safina iliyojengwa kwa ajili ya gharika, miaka mingi, mingi sana kabla gharika haijakuja, bali yeye alijua itanyesha. Biblia ilisema, ‘Kule kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule na Mungu atamwinua.’ Lini? Yeye hakusema. Mungu ni wa haki, Yeye ni wa kweli, soma tu jinsi Neno Lake lisemavyo.”

²⁹⁶ Hivyo ndivyo nimetenda usiku wa leo, kuwawekea wagonjwa mikono. Sasa, naamini kila mmoja wao ataponywa. Naamini, kila mmoja wao. Je, unaamini vivyo hivyo? Sasa amini kwa ajili ya hawa watu wanaoteseke.

²⁹⁷ Kuna maskini dada mmoja hapa, yaonekana kana kwamba namjua, nalimwobea usiku aliopita, kule katika mstari wa maombi. Jina lake ni nani? Chambers...Chembless. Kama maskini bibi huyo angaliishi—angaliishi kawaida hangaliteseka, bila shaka angalikuwa mwanamke mrembo. Naye ameketi pale sasa, akitetemeka. Roho ya kupendeza na nzuri katika msichana huyo. Naye ameketi pale akishtuka-shtuka hivi. Jamani, jinsi hiyo inavyouvunja moyo wangu. Jinsi ningalitaka sana...jinsi ningalitaka!

²⁹⁸ Hapa kuna mtoto mchanga, bibi ameketi hapa akimshika. Ulimi wake unaning’inia nje, maskini mwili wake mdogo unateseka. Vipi kama huyo alikuwa mtoto wangu Joseph? Vipi kama ingalikuwa mjukuu wangu Paulo? Vipi kama ni Rebeka anayeketi kule nyuma, au Sara? Vipi kama Bi Simpson hapa alikuwa mke wangu Meda? Huyu kijana mwanamume anayeketi hapa alikuwa Billy Paul? Mwanamke mkongwe anayeketi hapa alikuwa mamangu? Kumbuka, ni mtoto mchanga wa mtu fulani, dada wa fulani, binti wa fulani, mwana wa fulani. Mwaona? Mimi ni ndugu yao, yeye ni Mwokozi wetu. Yote niwezayo kufanya ni...imani niliyo nayo inatolewa kwa ajili yao. Hayo ndiyo yote nijuayo.

²⁹⁹ Naam, Bwana anaweza kunionyesha ono, Yeye angeliniambia shida ya kila mmoja wao. Naweza kuwathibitishieni ninyi hayo, mwaona, mnaajua hivyo. Bali hiyo haiwaponyi. Hiyo haiwaponyi. La, hapana budi kitu fulani kiwaingie, mwaona. Nami natumaini...

³⁰⁰ Kama vile ningekuja humu na kumchukua kila mmoja wenu na kuwabatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo, hilo halitawaondolea dhambi zenu. La, la! La, siamini katika ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo kwa kuzaliwa mara ya pili; naamini Damu ndiyo inaleta kuzaliwa mara ya pili, mwaona, si kule majini. Bali, mwaona, ningaliwabatiza na kuwabatiza, bali unazamishwa tu mwenye dhambi mkavu ukatoka ukiwa mwenye dhambi aliyelowa maji; waona, hata utakapotubu

kweli kweli. Tubuni, ndiposa mkabatizwe katika jina la Yesu Kristo. Mwaona? Hapo ndipo ninapohitilafiana na mafundisho ya dhehebu la Umoja. Si kubatiza kwa kuzaliwa mara ya pili, la; Damu ndiyo ioshayo, si maji. Mwaona? *Toba*, ndiposa ukabatizwe katika Jina la Yesu Kristo.

³⁰¹ Sasa nitashuka nikaombe. Na watu hawa walivyo kwenu ndivyo walivyo kwangu mimi, labda hata kuliko—kuliko watu wa jamii yangu.

³⁰² Sasa hebu tuungane pamoja, na mikono yenu kwa imani, na mikono yangu kwa imani, tukiishusha mikono ya Bwana Yesu ikawekwe juu ya maskini watu hawa walemavu. Je, mtaomba pamoja nami?

³⁰³ [Mahali patupu kwenye ukanda—Mh.] Wale walio na lesa ambazo ni za wagonjwa na wanaoteseka mnaweza kuzichukua mara baada ya ibada. Basi nisaidieni kuwaombea hawa, sivyo?

³⁰⁴ Mungu, tunakushukuru, Bwana, kwa ajili ya yale uliyofanya usiku wa leo. Tunakushukuru kimbele kwa uponyaji wa kila mtu aliyepishwa mstarini. Mungu mpendwa, naziombea hizi lesa, labda kwa wengine ambao hata hawangalikuja mkutanoni, na wapenzi wao wakaleta hizi lesa. Katika Biblia tunafundishwa ya kwamba wao walichukua kutoka mwili wa Paulo, lesa ama vijiitambaa. Basi, watu hao huko nyuma walikuwa wameishi katika uwepo Wako, walikuwa wamekuona barabarani, walikuwa wamekuona mikutanoni mwao, na waliona Roho Wako yule yule juu ya Paulo. Nao walijua haikuwa huyo mtu, ilikuwa Roho Wako aliyekuwa akiyatawala maisha yake, kwa kuwa tunamwona Paulo akitenda mambo yale yale uliyoyatenda.

³⁰⁵ Na sasa, Bwana, watu wa siku hizi wanamwona Mungu yule yule akiishi Kanisani Mwake pamoja na watu Wake. Nao wameleta lesa hizi, kusudi zipate kutolewa hapa zipelekewe wapenzi wao. Tujalie, Mungu, ili kila mmoja wao apate kuponywa jinsi upendavyo. Hatuombi jambo fulani lifanywe kwa njia yo yote ama kwa hali fulani; tunaomba tu, “Upendavyo, Baba, waponye.” Kwa utukufu wa Mungu, naomba ombi hili la imani juu yake. Katika jina la Yesu Kristo. Amina.

³⁰⁶ Nimekuwa na wakati wa ajabu wa ushirika katika imani yenu, kuwepo kwenu katika Yesu Kristo. Huu utakuwa mkutano ambao nitaukumbuka juu ya yale yaliyotendeka; upendo, kushirikiana, ushirika.

³⁰⁷ Basi, hata tutakapoonana tena, Mungu wa Mbinguni na awaongoze. Yeye yule anayefanya nyota zing’ae usiku kuangazia njia inapokuwa giza, na aangazie njia zenu kwa Nyota ya Bethlehemu kuwaongoza ninyi kufikia maisha yaliyosalimishwa kabisa katika Neno Lake, ndilo ombi langu.

Hata twonane huko juu,
 Hata twonane kwake kwema,
 Hata twonane huko juu,
 Mungu awe nanyi daima.

308 Sasa natusimame. *Yesu kwa Imani*...?...Mimi...vema,
 nitaubadilisha huo. Naamini hiyo ni sawa:

Yesu kwa imani
 Nakutumaini,
 Peke Yako,
 Nisikie sasa,
 Nakunitakasa,
 Ni wako kabisa
 Tangu leo.

309 Sasa na tusalimianeni kwa mikono wanapoimba:

Nipe nguvu pia
 Zakusaidia
 Moyo wangu;
 Ulikufa wewe
 Wokovu nipewe,
 Nakupenda wewe
 Bwana wangu.

310 Mnajisikia vyema sasa, sivyo?

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu,
 Ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua

Sasa juu ya mbawa za hua nweupe kama
 theluji,
 Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu,
 Ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

Sasa juu ya mbawa za hua nweupe kama
 theluji,
 Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu,
 Ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

311 Huo ndio ujumbe wetu wa mwisho wa kampeni hii:

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
 Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu,
 Ishara kutoka juu,
 Juu ya mbawa za hua.

312 Tuinamishe vichwa vyetu. Huku magurudumu yakivumisha
 wimbo kuelekea nyumbani, natumaini ita... mngesikia mvumo
 wa magurudumu, kunguruma kwa mtambo:

Juu ya mbawa za hua mweupe kama theluji,
Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu,
Ishara kutoka juu,
Juu ya mbawa za hua.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha hiyo pambio—Mh.] . . .
hua,

Mungu hutuma upendo Wake msafi na mtamu,
Ishara kutoka juu,
Juu ya mbawa za hua.

³¹³ Huku vichwa vyenu vimeinamishwa, nawakabidhini kwa . . .
Ndugu yenu Noel.



JUU YA MBAWA ZA HUA MWEUPE KAMA THELUJI SWA65-1128E

(On The Wings Of A Snow-White Dove)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Novemba 28, 1965, kwenye Maskani ya Uzima kule Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org